
epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 26, 2025 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com 0677 020 710
ISSN 0856 • No. 0581933

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




UKURASA WA 2

**Mtoto** aokotwa msituni, akutwa amedhoofika

UKURASA WA 3

**Maagizo** sita kwa Ma-DC mfumo wa taarifa za watu wenye ulemavu



UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO:

**Vijue** vifutio vya ndoto unazoota usiku

UKURASA 21

**Kimmich mambo safi Real Madrid**

## RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Rushwa ilivyoshamiri vituo vya ukaguzi polisi barabarani

UKURASA 4 & 5




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi zawadi kwa Mwanafunzi Bora wa Shahada ya Kwanza ya Sayansi katika Baiolojia na Kemia, Aisha Said, wakati wa Mahafali ya 24 ya Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait, Chukwani, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 3

## Dar na Zanzibar zaongoza biashara ya usafirishaji haramu binadamu

# Wakili mbaroni kwa tuhuma za utekaji

UKURASA 2



SACP Justine Masejo

**MICHEZO** **SIMBA: TUTACHEZA KAMA FAINALI LEO** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Mtoto aokotwa msituni, akutwa amedhoofika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MTOTO anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka miwili ambaye jina lake halijafahamika, amekutwa katika msitu wa Mkweni ulioko kati ya mkoani Shinyanga na Geita, akiwa amedhoofika mwili.

Amekutwa na wasamaria wema na tayari amekabidhiwa katika Kituo cha Kulelea Watoto Yatima Zaqahana kilichoko Mji mdogo wa Kagongwa, Manispaa ya Kahama.

Akizungumzia tukio hilo, Mwalimu Zakia Mwambiko, alisema walimpokea kutoka kwa maofisa ustawi wa jamii waliodai kuwa ameokotwa na watumishi wa Halmashauri ya Ushetu akiwa amelazwa kando ya barabara ya pori hilo.

Zakia alisema mtoto huyo amempatia jina moja la Bahati na kuwa kwa sasa hawezi kula zaidi ya kunywa maji na maziwa, hali iliyosababisha kuumwa mara kwa mara.

"Majibu ya daktari ni kuwa viungo vyake vina shida hali inayosababisha miguu kukosa nguvu ya kukanyaga chini ya ardhi. Shingo yake haitulii au kusimama kama watoto wengine. Haongei, ana uoni hafifu hali inayomsababishia kushindwa kulala na pia kupata choo," alisema.

Aliwaomba wadau kwa kushirikiana na serikali kuangalia namna ya kumpeleka mtoto huyo katika hospitali kubwa zenye madaktari bingwa kuchunguza afya yake.

Mkurugenzi wa The Little Ones Charity Plus Foundation, Mhandisi Manyango Barnabas, alisema kitendo alichofanyiwa mtoto huyo ni ukatili ambao haupaswi kuvumilika ndani ya jamii.

Barnabas aliunga mkono kazi kubwa inayofanywa na kituo hicho kwa kutoa msaada wa mafuta ya kula, mchele, maharage, sabuni, madaftari, dawa za meno na miswaki, mahindi, unga wa sembe na ngano.

Mkazi wa Kagongwa, Jane Haule, alisema ugumu wa maisha katika familia unasababisha baadhi ya wazazi kuzikimbia familia zao na wakati mwingine baba kukataa ujauzito au mtoto kukataliwa anapozaliwa.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, akizungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali kutoka Kanda Maalum ya Dar es Salaam juzi, ambao watwaimarisha usalama wakati wa Mkutano wa Nishati, utakaowakutanisha wakuu wa nchi zaidi ya 51 na mawaziri wa fedha na nishati 60 wa Afrika, kesho na keshokutwa. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Wakili mbaroni tuhuma za utekaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu wawili, akiwamo wakili wa kujitegemea, kuhusiana na taarifa zilizosambaa katika mtandao wa kijamii zinazoeleza kunusurika kuuawa, kutekwa na kupigwa nyundo kichwani raia wa Afrika Kusini, Suzan Shawe (75).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, katika taarifa yake jana, aliwataja watuhumiwa hao ni Qamara Valerian (36) ambaye ni Wakili wa Kujitegemea na Benjamin Paul (19) dereva pikipiki (bodaboda).

"Raia huyu wa kigeni alivamiwa nyumbani kwake eneo na Njiro, Block C1, Januari 21, mwaka huu, saa 3:00 asubuhi na watu waliotumwa na Valerian kwa nia ya kumtoa kwa nguvu kwa madai ya kutolipa kodi ya nyumba hiyo anayoishi," alisema.

Kamanda Masejo alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea na mara baada ya upelelezi kukamilika taratibu nyingine za kisheria zitafuata.

Alisisitiza umuhimu wa wananchi kufuata sheria na kanuni katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.

Kadhalika, alitoa rai kwa baadhi ya waandishi wa habari mkoani Arusha kufanya uchunguzi wa taarifa zao na kujiridhisha kabla ya kuzitoa ili kuondoa taharuki kwa wananchi na wageni wanaofika katika mkoa huo.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake Njiro, Susan alidai saa 3:00 asubuhi akiwa hapo walifika watu asiowafahamu wakiwa na pikipiki sita walizokuwa wamepakizana watatu watatu na kuvamia nyumba hiyo ambayo amepangisha na ameishi hapo kwa zaidi ya miaka 20 sasa.

Alisema watu hao walikuwa na kiongozi wao waliokuwa wakimwita kwa jina moja la Abdul ambaye alikuwa akiwashurutisha wenzake kumtoa ndani ya nyumba hiyo kwa nguvu.

"Nilikuwa chumbani kwangu nikasikia kelele, msichana wangu anayenisaidia kazi za nyumbani alikuja na kuniambia kuna tatizo kubwa nje.

Nilipofunga mlango wangu kwa komeo na baada ya muda mfupi nilisikia mlango ukivunjwa na watu hao wakiongozwa na Abdul wakaingia chumbani," alisema.

Alisema walipoingia walimkamata na kumpeleka bafuni kisha wakaanza kumpiga, huku mmoja alimpiga kwa nyundo kichwani.

Alidai kuwa walimvua nguo na kumburuza kutoka ghorofani hadi getini akiwa utupu, wakimsisitiza atoke ndani ya nyumba hiyo kwa sababu anadaiwa kodi.

"Nipo hapa nchini kwa ajili ya kufuatilia mirathi ya marehemu wangu aliyefariki dunia miaka miwili iliyopita na tumeishi naye hapa kwa zaidi ya miaka 20 tukiwa wapangaji na tumepangishiwa nyumba hii na Irene Sianga anayeishi nchini Uingereza.

"Tumepangishwa kwa makubaliano ya kumlipa kiasi cha Dola za Kimarekani 800 na nimekuwa nikilipa kila mwezi na nimemlipa fedha mwanzoni mwa mwezi huu," alisema.

Alidai wakati wanaendelea kumshurutisha atoke kwenye nyumba hiyo, baadhi ya watu walibaki chumbani kwake wakipekua na kuchukua vitu mbalimbali zikiwemo fedha.

Mfanyakazi wa Suzan, Ayubu Malolo, alisema wakati akiendelea na majukumu yake nyumbani hapo lilifika kundi la watu wakiwa wamepakizana kwenye bodaboda wakiwa na mapanga na nyundo na kumwuliza sababu za kuishi katika nyumba hiyo bila kodi.

"Kabla sijawajibu walinitaka niwapeleke kwenye chumba cha bosi wangu huku kiongozi wao aitwaye Abdul akitangulia na kwenda kuwafungia mbwa kwenye banda kwa komeo walioukuwa wakipiga kelele," alidai.

Mfanyakazi huyo alidai alipowafikisha ghorofani na kuwaonesha chumba cha bosi wake walimweka chini ya ulinzi na kisha wakavunja mlango wake na kuingia chumbani kwake.

# Ongezeko samaki Ziwa Tanganyika lachochea uwekezaji

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji, amesema upumzishwaji wa hiari wa shughuli za uvuvi wa Ziwa Tanganyika umechagiza ongezeko kubwa la malighafi kwa ajili ya viwanda vya kuchakata vilivyoko kwenye mikoa inayolizunguka.

Alisema hayo juzi baada ya kutembelea na kukagua kiwanda cha kuchakata samaki cha Alpha Tanganyika kilichoko mkoani Rukwa.

Dk. Kijaji alisema hivi sasa samaki wameongezeka kutoka tani 4,700 zilizokuwa zikizalishwa 2023 na kufikia tani 15,000, ambapo ongezeko hilo limesaidia wafanyabiashara hadi kukosa masoko ya kupeleka.

Kutokana na hali hiyo, kiongozi huyo alimtaka mwekezaji wa kiwanda hicho kuanza shughuli za uchakataji mara moja na kwamba, serikali itabeba changamoto za kisera ili kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa mazuri.

"Tunataka viwanda vitengeneze ajira kwa vijana wetu na ninajua hapo awali sababu yako kubwa ilikuwa ni kutopata malighafi za kutosha kulingana na uwezo wa kiwanda chako, lakini kwa sasa kupitia upumzishwaji wa ziwa, samaki wameongezeka," alisema.

Mmiliki wa kiwanda hicho, Alpha Nondo, mbali na kuishukuru serikali kwa ushirikirikano, alisema kiwanda chake kitakuwa cha kwanza nchini kuchakata samaki kutoka Ziwa Tanganyika na Victoria kwa wakati mmoja.

"Tayari tuna ithibati kutoka masoko ya Umoja wa Ulaya na Marekani, hivyo tunaamini tukianza kazi uchumi wa watu wa Mkoa wa Rukwa utaimarika," alisema Nondo.

## HABARI KITAIFA

# JK asisitiza elimu ya msaada kisheria

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, amesema bado kuna umuhimu mkubwa wa utoaji elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi.

Amesema ni muhimu ili kusaidia kuwapo na utawala wa kisheria na haki katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hivyo, amezitaka taasisi zote zinazosimamia haki ambazo zinashiriki wiki ya sheria, kuhakikisha zinatenga muda wa kusikiliza kero za wananchi ikiwamo kuzipatia ufumbuzi kwa msaada wa kisheria.

Kikwete aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa Wiki ya Sheria inayofanyika viwanja vya Nyerere, jijini hapa.

Alisema kuna mambo mengi ya msingi katika sheria ambayo wananchi wanapaswa kujifunza,ikiwamo kupewa elimu, kwa sababu jamii ikikosa utawala wa kisheria na haki haiwezi kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Nawapongeza sana kwenye hili la uwapo wa wiki ya sheria, kwa sababu ukiacha mambo mbalimbali mnayofanya wiki hii, mnaitumia pia katika kujitathmini katika utendaji wenu wa kila siku katika utekelezaji wa majukumu yenu," alisema Kikwete.

Alisema katika utoaji elimu ambao wanafanya, wanapaswa kuzingatia elimu ya mifumo ambayo hutumika katika utoaji haki na kwamba, wananchi wakipata uelewa katika hilo itakuwa rahisi kuelewa mambo mbalimbali ya kisheria.

Alibainisha kuwa wiki hiyo ni muhimu kuwapo kwa sababu itawasaidia wananchi kupata uelewa kwenye sheria na kuibua mambo mbalimbali ya msingi ambayo yanaweza kuboresha kwa kuzingatia mahitaji ya umma.

Hata hivyo, alisema kupitia njia hiyo ya utoaji elimu kutasaidia kupatikana kwa taarifa mbalimbali kuhusu ukiukwaji wa haki unaofanywa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kikwete aliwapongeza mafanikio makubwa yanayoonekana katika utendaji kazi wao hususani kwenye suala zima la uboreshaji mahakama ikiwamo katika matumizi ya masuala ya TEHAMA katika uendeshaji kesi. Kuhusu ushiriki kwenye Dira ya 2050, alisema ni vyema taasisi zote zinazohusika na utoaji haki zikashiriki kikamilifu katika kutoa mchango kwenye dira ya Maendeleo ya mwaka 2050 ambayo inaanza kutekelezwa Januari mwakani.

Awali, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania Prof. Ibrahim Juma, alisema wiki hiyo hutumika kutoa elimu ya sheria kwa jamii ili kufahamu katiba, kanuni na taratibu za shughuli za mahakama na haki jinai zinavyokwenda.

Prof. Juma alisema kilele cha wiki hiyo kitakuwa Februari 3, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, alielekeza mahakama na taasisi zake zote zinazohusika na utoaji haki zifanye maboresho katika utekelezaji wa Dira ya 2050.

Alisema Wiki ya Sheria itumike kukumbushana kuhusu mambo mapya ya utekelezaji wa Dira ikiwamo utawala bora, amani na utulivu kwa kuangalia sheria, sera na miongozo.

# Dar, Zanzibar zaongoza biashara ya usafirishaji haramu binadamu

**Na Restuta James**

MTANDAO wa Wanaharakati wanaopinga usafirishaji haramu wa binadamu (TANAHUT), umetaja mikoa inayoongoza kwa biashara hiyo huku visiwa vya Zanzibar na Dar es Salaam, ikiongoza.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa mafunzo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DarTU) ili kuwajengea uelewa, Mkurugenzi Mtendaji wa TANAHUT, Wakili Edwin Mugambila, alitaja mikoa mingine ni Singida, Tabora, Shinyanga, Geita, Mwanza, Iringa, Manyara, Tanga, Mtwara, Arusha, Songwe, Mbeya, Kagera na Kilimanjaro.

Alisema visiwa vya Zanzibar ni lango kuu wakati Dar es Salaam ni mji wenye kazi nyingi za kutumikisha mabinti na watoto hasa biashara haramu ya ngono.

"Zanzibar ni lango kuu na Dar es Salaam ndio kitovu chenyewe. Dar es Salaam kuna biashara ya ngono inaendelea, kuna viwanda, uvuvi na biashara kubwa ya ngono na ndio maana unaona kuna massage spa na madanguro kila mahali," alisema.

Alisema kwenye vituo vya mabasi, mtandao huo unashuhudia utumikishwaji wa watoto kwenye biashara ndogo ndogo na kwamba wengine kwenye viwanda, migahawa na hoteli.

Mikoa ya Geita, Shinyanga na Tabora, alisema kuna utumikishwaji wa watoto kwenye mashamba makubwa ya tumbaku na migodini, ambako pia kuna biashara haramu ya ngono.

Aidha, alisema kwenye baadhi ya mikoa, watoto wa kike na wa kiume pamoja na mabinti, wanarubuniwa na kusafirishwa kwenda kwenye miji mikubwa kwa ahadi ya kazi halali, lakini wanaishia kutumikishwa kwenye ngono.

Mugambila alisema ili kukabiliana na usafirishaji haramu, TANAHUT inatumia mbinu ya kuzuia, kuwalinda waathirika na kuwashitaki wahusika.

Aliitaka jamii iungane kupinga biashara hiyo ili Tanzania iwe sehemu salama kwa ustawi wa watu wote.

Mkurugenzi wa Programu wa TANAHUT, Jones John, alisema tatizo hilo linahitaji nguvu za pamoja kulikabili.

Alitoa rai kwa wanafunzi wanaochukua Shahada za Uzamili na Uzamivu, kufanya utafiti na kutoa maandiko ya kitaaluma, yatakayosaidia taifa kuondokana na tatizo hilo, linaloathiri zaidi wanawake na watoto.

"Tunashirikisha walimu na wanafunzi ili kwa pamoja waone kuna uwezekano gani kuingiza tatizo hili kwenye masomo yao ili kuchechemua hamasa ya wanafunzi na jamii nzima kufahamu tatizo hili," alisema.

John alisema lengo la wanaharakati kushirikiana na vyuo ni kutengeneza kizazi cha wadau wengi wenye uelewa ambao wanaweza kutumia elimu yao kulitafutia ufumbuzi.

Mkurugenzi wa Nyumba Salama (Courage Worldwide), Suzan Shoo, alisema waathirika wakubwa wa biashara hiyo ni wanawake na watoto, kutokana na kwamba ni makundi yasiyo na sauti wala nguvu ya kujitetea.

"Usafirishaji haramu wa binadamu unatokea kwenye jamii yetu. Wengi wanadhani unatokea nje ya nchi kumbe unatokea mitaani na kwenye vijiji vyetu. Tunahitaji nguvu ya pamoja kulikabili," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akionesha kishikwambi alichokabidhiwa, baada ya kuzindua Kanzidata na mfumo wa taarifa za watu wenye ulemavu unaotokana na Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, jijini Dodoma, jana. Wengine ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia) na (wa pili kushoto) ni Mhasibu wa Bendi ya watu wenye ulemavu ya Jumuiya, Hemedi Ilimbo. **PICHA: OWM**

# Maagizo sita kwa Ma-DC mfumo taarifa za watu wenye ulemavu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo na maelekezo sita kuhusu mfumo wa taarifa za watu wenye ulemavu kwa wakuu wa wilaya ikiwamo kuhakikisha ofisi za ustawi wa jamii katika halmashauri zinawapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi wenye ulemavu.

Amesema kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, asilimia 11.2 ya watu wote nchini wana ulemavu wa aina fulani huku Zanzibar ikiwa na asilimia 11.4 ambapo idadi kubwa zaidi ni wanawake kwa asilimia 11.6 na asilimia 10.9 ya wanaume.

Akizindua mfumo huo jana jijini hapa, Majaliwa alisema ni mara ya kwanza Tanzania kuuandaa na ni nyenzo muhimu kwa serikali, wadau wa maendeleo na watunga sera katika kupanga, kutekeleza, na kufuatilia maendeleo ya watu wenye ulemavu nchini.

Waziri Mkuu alisema matokeo ya sensa yanabainisha ulemavu wa kuona ndio unaoongoza ukiwa na asilimia tatu ya watu wote wenye ulemavu.

"Kiwango hiki kinafuatiwa na ulemavu wa kutembea asilimia 1.8 na ulemavu wa kusikia asilimia 1.1 na watu wenye ualbino asilimia 0.1," alisema.

Majaliwa alizitaka taasisi zote za umma, sekta binafsi, asasi za kiraia na wadau wa maendeleo kushirikiana na serikali katika kutumia mfumo huo kikamilifu kwa kufanya muamuzi wenye vigezo vya kitakwimu katika kupanga na kufuatilia utekelezaji wa sera, mipango na afua mbalimbali zinazolenga kukuza na kuimarisha maendeleo ya watu wenye ulemavu.

Pia alisema Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara (SHIVYAWATA) na Shirikisho la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu, Zanzibar (SHIJUWAZA) watumie takwimu hizo kuhuisha kanzidata zao.

"Taasisi zote zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu tumieni takwimu hizi katika kutayarisha programu za kuwawezesha na kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali na wadau wa maendeleo kujiendeleza kiuchumi, kijamii na mazingira," alisema.

Aliwataka wazazi na walezi wote wasiwafiche watoto na watu wenye ulemavu na wahakikishe wanafahamika mahali walipo pamoja na hali zao za ulemavu.

Alisema lengo ni kupata huduma stahiki huku akiwataka watekelezaji na wasimamizi wa miradi mbalimbali ya ujenzi wahakikishe uwapo wa miundombinu sahihi kwa ajili ya watu hao.

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Hivi ndivyo rushwa ilivyoota mizizi ukaguzi barabarani

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** KIGOMA



Mmoja wa askari wa usalama barabarani akipokea pesa ya 'ushirikiano' kutoka kwa kondakta katika moja ya vituo vya ukaguzi barabarani mkoani Kigoma kama alivyonaswa na mwandishi wa ripoti hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

ZIKIWA zimepita wiki kadhaa ikishuhudiwa kusambaa kwa picha jongefu za askari wa usalama barabarani wakipokea rushwa hadharani kisha kuchukuliwa hatua, hali ya namna hiyo ni ya kawaida kwa muda mrefu mkoani Kigoma na imekuwa kama utaratibu wa kawaida na halali.

Askari wa usalama wa barabarani kutumia vituo vya ukaguzi kama sehemu ya kitegauchumi wakitoza fedha kwa kila gari linalopita kinyume cha utaratibu huku wakiita utaratibu huo kuwa ni pesa ya 'ushirikiano'.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura Namba 329 marejeo ya mwaka 2022 kifungu namba 15, hatua yoyote ya kuahidi, kutoa, kupokea au kushawishi moja kwa moja au kupitia kwa wakala, kitu chochote cha thamani ili kupindisha utaratibu katika utoaji wa uamuzi inatafsiriwa kuwa ni rushwa.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inataja rushwa ni hatua na athari ya ufisadi, ambayo ni mchakato wa kuvunja kwa makusudi utaratibu wa mfumo, kimaadili na kiutendaji kwa faida ya kibinafsi.

TAKUKURU inaenda mbali zaidi na kubainisha kuwa mbali na mafisadi kufanya kitendo kisicho halali, pia wanashinikiza au kulazimisha wengine kufanya vitendo kama hivyo.

**KINACHOENDELEA**

Katika safari ya kilometa 27 aliyoifanya mwandishi wa ripoti hii kutoka Kigoma Mjini mpaka eneo la Mkuti, kwenye vituo saba vya ukaguzi ambako anashuhudia kila kituo, msaidizi wa dereva anashuka kupeleka 'makusanyo' kwa askari na gari kuruhusiwa kupita bila kufanyiwa ukaguzi.

Fedha anazozibaini zikitolewa katika kila kituo ni kuanzia Sh.2,000 mpaka 5,000, bila maandishi yoyote wala risiti hali inayotajwa kuwa sehemu ya upotevu wa mapato ya serikali kwa kuwa fedha hizo zinaishia katika mifuko ya watu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Umoja wa Wasafirishaji Kigoma (KIBOTA), zaidi ya magari 1,190 yanalazimika kutoa hongo kila yapitapo kwenye kila kizuizi.

Magari hayo yanajumuisha daladala 867, mabasi madogo 123, michomoko na Toyota Wish 200 pamoja na magari binafsi yanayofanya safari kati ya wilaya za Kigoma, Kasulu, na Uvinza.

Kwa hesabu ya kila gari kutozwa wastani wa Sh.2,000 kwa kila kituo katika vituo saba ni sawa na Sh.14,000 na magari 1,190 kwa hesabu hiyo, yanatoa zaidi ya Sh. milioni 16.6 kwa siku, kwa mwezi zaidi ya Sh. milioni 499.8 ambazo haziingii katika mifumo rasmi ya ukusanyaji mapato.

Fedha hiyo ambayo hupotea kila siku katika vizuizi vya ukaguzi vya polisi wa usalama barabarani vilivyoko barabara kuu iendayo Kasulu kutoka Kigoma Mjini kwa siku moja, ingeweza kutumika kujenga darasa moja la shule ya msingi lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 40 na kupunguza uhaba wa madarasa unaoikumba jamii ya mkoa huo.

Aidha, fedha hiyo kama ingekuwa kwenye ukusanyaji wa utaratibu maalum na wa kisheria, ingeweza kutumika kufanya marekebisho ya barabara hizo.

Kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Kigoma umeeleza kutumia zaidi ya Sh. milioni 17 katika marekebisho ya miundombinu ya barabara iliyoharibiwa ikiwamo uharibifu wa tabaka la juu la lami na uharibifu wa makalavati na mitaro.

Katibu wa KIBOTA, Nuru Hussein, anakiri barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 90, kilometa 27 za awali kuna zaidi ya vizuizi saba.

Anasema katika barabara hiyo, kuna vituo vya ukaguzi vya Stendi Mpya ndani na nje - kwa Mganza (Kazegunga), Nyangwe, Simbo, Mkuti na Baraka Sekondari. Vyote hivyo vimo ndani ya kilomita 27 kutoka Kigoma Mjini sambamba na magari ya ukaguzi wa madeni huku eneo la Kazegunga likigeuka kuwa sehemu maarufu ya ukaguzi unaotawaliwa na rushwa.

"Katika kila kizuizi na gari la ukaguzi, kila gari hulazimika kutoa kati ya Sh. 2,000 hadi 5,000 kama pesa ya ushirikiano, hii ni mbali na ushuru wa kawaida, kwa hiyo kwa siku dereva anaweza kutoa kati ya Sh. 15,000 na 20,000 ya 'ushirikiano'. Hii inatuumiza sana" anasema.

Madereva, anasema halazimika kutoa pesa hizo ili kuepuka usumbufu au adhabu zisizo za haki kwa kuwa madereva wanaoshindwa kutoa fedha hizo, mara nyingi hukumbwa na adhabu kubwa kama faini au kucheleweshwa safari, hali inayowaathiri kiuchumi, huku baadhi ya madereva wakilazimika kujaza abiria kupita kiasi ili kufidia gharama hizo.

Katibu huyo anasisitiza kuwa katika barua yao ya Mei 30, 2024 yenye kumbu Na KBT/KG/ML/VOL/30/2024 kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma walilalamika kuhusu ongezeko la vizuizi vya polisi katika barabara hiyo.

Anasema katika barua hiyo, waliomba kupunguzwa kwa vizuizi kwa madai kuwa ongezeko lake ni ishara ya kukithiri kwa rushwa ambayo dereva na kondakta wanapaswa kulipa.

Katika uchunguzi huo, mwandishi anabaini utaratibu huo ni wa kawaida na uliozoeleka kwa wasafirishaji hao. Katika kituo cha kwanza, kondakta anaonekana kushuka mkononi akiwa ameshikilia kitu na kwenda kwa askari ambaye anapokea kama salamu na kuruhusu gari kupita.

Kinachobainika pia katika vizuizi hivi, kuna kiwango maalum wanachokihitaji askari hao kwa kuwa katika kituo kimoja, mwandishi licha ya kutokusikia sauti ya kinachozungumzwa, anabaini askari akichukua fedha kisha kurejesha chenji.

Mwenyekiti wa daladala, maarufu kama michomoko, Sinda Zacharia, anasema suala hilo limedumu kwa zaidi ya miaka 10 na hakuna mabadiliko yoyote, hata yakitokea hudumu kwa muda mfupi.

"Imefika hatua tumezoea hii hali. Tuwe na hela tusiwe nazo tunafanya maandalizi ya fedha ya 'ushirikiano' ili asubuhi tukipita tuwaachie kwa sababu tusipofanya hivyo hali inakuwa mbaya barabarani.

"Matrafiki wana daftari la orodha ya madereva wanaopita katika barabara hiyo. Wanaweka kumbukumbu nani kalipa na nani hajalipa. Ambaye amelipa anaachiwa huru ambaye hajalipa anapaswa kulipa au la ataandikiwa faini hata kama kosa lake ni la kupewa elimu ili kumkomesha na kumrejesha kwenye pesa ya 'ushirikiano," anasema kiongozi huyo.

Msimamizi wa usafirishaji mkoa (jina linahifadhiwa kwa sababu za kiusalama), anasema rushwa kati ya madereva na makondakta na trafiki iko pia kwa mabasi yanayofanya safari nje ya mkoa. Basi haliruhusiwi kuondoka bila kuacha Sh. 20,000 kwa askari anayefanya ukaguzi.

"Ukifika stendi saa 10:00 alfajiri utaona hiki ninachokisema. Askari anakaa ndani ya gari hashuki, anasubiri kupelekewa Sh. 20,000 ndipo anashuka na kufanya ukaguzi abiria wakiwa wameshapanda mabasi," anabainisha.

Pia anasema kwa mabasi ambayo yanashindwa kulipa, abiria wanashushwa na kufaulishwa kwenye mabasi mengine, hivyo kutokuruhusiwa kuendelea na safari.

**RPC ANENA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Philemon Makungu anasema tuhuma hizo hazijafikishwa ofisini kwake na kwamba atalifanyia kazi kubaini ukweli wake.

"Kila mtu atimize wajibu wake badala ya kutuhumiana. Kama yupo mwenye kuthibitisha hilo anapaswa kutoa taarifa ili sheria ichukua mkondo wake kwa kuwa usalama barabarani unaongozwa na sheria," anasema Makungu.

Kuhusu ongezeko la vizuizi, anasisitiza kuwa vinaboresha hali ya ulinzi na usalama barabarani na vimesaidia kupunguza ajali licha ya kutokutoa takwimu kuonesha kupungua huko.

Makungu anawataka wananchi kutoa taarifa ya vitendo viovu vinavyofanywa barabarani ili jeshi liweze kuchukua hatua na kwamba ipo namba ya simu iliyotolewa kwa ajili ya kushirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu kama hayo hivyo wasikae kimya.

"Tunataka wananchi wahudumiwe vizuri, hatuwezi kufumbia macho vitendo viovu vinavyofanyika katika vizuizi vyetu, wananchi watoe taarifa ili sheria ziweze kuchukua mkondo wake," anasema Makungu.

Pamoja na kauli ya Kamanda

INAENDELEA UK. 5

# Hivi ndivyo rushwa ilivyoota mizizi ukaguzi barabarani

INATOKA UK. 4

Makungu, suala la vizuizi kuwekwa katika barabara hiyo halijazuia kutokea kwa ajali za mara kwa mara.

Taarifa kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, zinabainisha kuwa kwa mwaka 2023 pekee, kulikuwa na majeruhi 408 na vifo tisa vilivyotokana na ajali za barabarani na hadi kufikia Agosti, 2024 tayari kulikuwa na majeruhi 411 na vifo vya watu wanane.

Kadhalika takwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani ya Januari mpaka Desemba 2023, katika mikoa ya kipolisi Tanzania, mkoa wa Kigoma ulikuwa na matukio ya ajali 61, ajali na vifo 40, ajali za majeruhi 19 na ajali za kawaida mbili, katika ajali hizo walifariki watu 52 na waliojeruhiwa kuwa 78.

Taarifa hiyo imeeleza chanzo cha ajali kuwa ni kuchangiwa na ubovu wa magari kwa asilimia 4.1, hali inayoonesha kuwa vyombo hivyo havikaguliwi ipasavyo.

Kuhusu ukaguzi wa magari kila asubuhi, Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Kigoma, Addo Msigala, anasema wanafanya hivyo mara kwa mara ili kuhakikisha sheria ya usalama barabarani zinazingatiwa.

Anasema kutokana na ukaguzi huo kwa kipindi cha Januari hadi Novemba 2024 madereva walikokiuka sheria waliadhibiwa kwa makosa mbalimbali yanayohatarisha usalama barabarani yakiwamo kuvaa sare chafu (12) kuchanganya mizigo na abiria(saba) na abiria,kutotoa tiketi(14) na kusimamisha abiria (20).

Kanuni za ukaguzi wa magari ya mwaka 2023 zinaelekeza kuwa mkaguzi anatakiwa kutoa orodha ya kasoro na muda wa kuzirekebisha, lakini hali ni tofauti kwenye barabara ya Kasulu ambako askari anasimamisha gari na kumsubiri dereva ashuke na kumfuata alipo.

**TAKUKURU YATHIBITISHA**

Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma kutoka TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, Ibrahim Sadick, anasema asilimia 67 ya maoni ya wananchi yaliyokusanya kwa kipindi cha Machi, 2023 hadi 2024, yanaonesha rushwa imetawala utendaji wa polisi wa usalama barabarani.

Kadhalika, ripoti ya Kupambana na Rushwa Barabarani kwa Mwaka 2023 kipengele cha rushwa barabarani, Jeshi la Polisi lilirekodi matukio 1,250 ya rushwa barabarani, ikilinganishwa na matukio 1,100 yaliyoripotiwa mwaka 2022.

Pia utafiti wa uliofanywa na TAKUKURU 2022/23 ulilitaja Jeshi la Polisi kuwa msatari wa mbele likiwa na 55.6 kati ya vinara wanne.

**MADEREVA WANG'AKA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hii, baadhi ya madereva ambao hawakupenda kutajwa majina yao na wadau wengine wa usalama barabarani, wanasema rushwa inaathiri maisha ya jamii na kukiuka misingi ya utawala bora.

Dereva wa kwanza analalamika kuwa anapata kipato kidogo na hivyo kushindwa kuhudumia familia yake ipasavyo na kuzua ugomvi nyumbani kwake huku mke wake akimtuhumu kwa matumizi mabaya ya pesa.

"Kwa mzunguko mmoja tunapata Sh. 112,000 ambayo nalipa pesa ya chama Sh. 2,000, mafuta naweka ya Sh. 60,000, mwenye gari namlipa Sh. 40,000, ushuru Sh. 1,000/= na 'ushirikiano' Sh. 15,000. Pesa yote inaisha ili nipate ziada inabidi nijaze abiria zaidi au nipakie mizigo," anasema dereva huyo.

Dereva mwingine anasema wanaposhindwa kulipa pesa ya 'ushirikiano', askari wanawalipa visasi na kuwaita majina magumu kama "jiwe" au "nati" na hata kuwabambikia makosa ili walipe faini ya Sh. 30,000 kwa kosa ambalo lingehitaji elimu peke yake.

Katibu Tawala Msaidiai anayeshughulikia Mipango na Uratibu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Frank Makua, anasema kutokana na rushwa serikali inaweza kupoteza wawekezaji ambao wataingia mkoani Kigoma na kuufanya mkoa huo kuwa kitovu cha biashara kama inavyokusudiwa.

Pia anasema wafanyabiashara wengi watakimbia kufanya biashara ambazo zinawaingizia hasara na kuanza kufanya biashara za mitandao ambapo serikali itapoteza kodi na hivyo kuathiri miradi ya maendeleo.

"Mapato yanayochepushwa yanachangia kutofikiwa kwa malengo ya utekelzaji wa miradi ya maendeleo na kuondoa umaskini kama ilivyoanishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) lengo la kwanza la kutokomeza umaskini kwa kila hali.

ITAENDELEA...



Msemaji Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa akizungumza na waandishi wa habari, katika Hifadhi ya Taifa Mikumi, mkoani Morogoro jana, kuhusu mipango ya maendeleo ya serikali. Habari Uk. 8. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri apiga kambi mipakani kuelimisha masuala ya kisheria

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ameongoza jopo la wataalamu wa msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) kutoa huduma na elimu ya uraia kwa wananchi.

Wananchi hao ni kutoka kata ya Kibirizi iliyoko Manispaa ya Kigoma Ujiji, mkoani Kigoma, kutokana na baadhi kukabiliwa na utata wa uraia wanapohitaji kupata vitambulisho vya uraia (NIDA).

Dk. Ndumbaro ambaye yuko mkoani humo jana alikuwa katika kata hiyo kusikiliza na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu changamoto za masuala ya kisheria.

Kampeni hiyo ambayo imeanza juzi mkoani humo imelenga kuvifikia vijiji 240 mkoani humo.

Waziri huyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza wananchi wapewe elimu hiyo sambamba na elimu ya sheria na katiba, haki za binadamu na msaada wa kisheria ili wajue sheria na kupata haki zao.

"Tanzania ni nchi nzuri yenye kuvutia wema na wabaya, yenye neema kedekede, sisi tumejaa neema, ina amani na utulivu na mfumo mzuri wa maisha, kuna nchi hazina haya tuliyo nayo.

"Uzuri huu unawavutia wengi, wengine wanakuja kwa kufuata taratibu rasmi za uhamiaji, wapo wanaokuja kwa njia za panya, hawa ndio wanaotuponza,"alisema.

Alisema wananchi wa eneo hilo wanapaswa kuwa makini kwa kuwa tatizo hilo la mipakani kuna kuingiliana kwa makabila na nchi jirani.

"Juzi tulikuwa na kesi moja kuna raia wa Burundi walikaa huku wakapewa uraia, mmoja aliyepewa uraia ameenda Burundi anaongoza chama cha siasa. Tunamjua kama Mtanzania, lakini nchi jirani anaongoza chama cha siasa hiyo ni sawa? Hapa ndipo mgogoro unapokuja," alisema.

Waziri Ndumbaro alisema katika kampeni hiyo, Kigoma watatoa elimu ya uraia kwa kuwa masuala ya uraia ni magumu hasa maeneo ya mipakani.

"Lazima tufahamu sheria, suala si kuzaliwa tu, endapo ulizaliwa na mmoja wa wazazi sio Mtanzania unapaswa ufanye nini kwa mujibu wa sheria. Unakwenda uhamiaji unasema 'baba yangu alikuwa Mrundi na mama yangu Mtanzania, nimefikisha umri wa miaka 18 ninachagua sasa kuwa Mtanzania naomba mnihalalishe'," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema gharama za huduma za kisheria ni kubwa ndio sababu iliyomsukuma Rais Samia kubuni kampeni hiyo ili kuwasogezea wananchi huduma za kisheria popote walipo.

"Wataalamu hawa wako kwenye kata 80 na vijiji 240 wanaendelea kusikiliza na kutatua kero za kisheria za wananchi wa Kigoma," alisema.

Mbunge wa Kigoma Mjini, Kilumbe Ng'enda, alisema ni maono ya Rais Samia kuhakikisha wananchi wanapata nafasi ya kusikilizwa na kupata msaada wa kisheria.

"Wananchi hawa wana kadhia nyingi zinazotokana na mambo ya sheria kuhusu hukumu zinazotolewa na katika mahakama, nakala za hukumu, namna ya kusikiliza mashtaka, upelelezi, kukaa muda mrefu rumande, umiliki wa viwanja," alisema.

Alisema pamoja na matatizo mengine ya kisheria yaliyoko Kigoma Mjini kuna suala la utata wa uraia wa watu.

"Kuna watu mababu zao wamezaliwa Kigoma na wamefia Kigoma, msaada wa kisheria namba moja tunaohitaji ni kutatua utata wa uraia wa watu. Watu wameomba namba za NIDA hawajapata, wamepeleka hadi wazazi wao, lakini bado wameonesha na makaburi ya wazazi wao, lakini bado wanapata misukosuko," alisema.

Alisema kuna tatizo la watu kuhusisha kabila na taifa na kwamba, msaada huo wa kisheria utatoa tabasamu kwa wananchi ambao wamekosa watu wa kuwatetea katika changamoto zao za kisheria.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watu wanaotaka kutumia dini kuvuruga amani wasivumiliwe

**WIKI** hii, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete alihudhuria kikao cha Kamati ya Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT) na kuwaonya Watanzania kuacha kutumia mwamvuli wa dini kujenga chuki na mifarakano katika jamii hali inayochochea machafuko na uvunjifu wa amani.

Licha ya kutoa onyo hilo, aliwataka viongozi wa dini kusimama imara kuhakikisha Tanzania inaendelea kubaki kuwa kisiwa cha amani, utulivu, umoja na mshikamano. Pia aliwakumbusha kwamba amani na utulivu kamwe haviwezi kununuliwa dukani, hivyo ni lazima Watanzania waendelee kuimarisha undugu na mshikamano na kuepuka kubaguana kwa misingi yoyote ikiwamo ya kiimani, rangi na ukabila.

Kikwete ambaye ni mwasisi wa jumuiya hiyo, alikumbusha kuwa chachu ya kushauri kuanzishwa kwa taasisi hiyo enzi za serikali aliyoiongoza, ilisababishwa na mgogoro wa kidini ulioibuka wa kuchinja, kati ya waumini wa Kiislam na Kikristo. Alisema licha ya kuanzia eneo dogo la Katoro mkoani Geita, watu waliusambaza na kuuchochea kuwa wa kiimani na kusababisha machafuko, mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali.

Kutokana na kuwapo kwa mgogoro huo, Kikwete alisema hali ilikuwa mbaya kwa kuwa kila mmoja alichukua upande wake, ikabidi serikali ianze kuwadhibiti watu na vyombo vya habari vilivyoonekana kuuchochea. Pia alisema ilibidi serikali kuitisha mkutano uliowahusisha viongozi wa dini zote wakala na kunywa pamoja ili kila mmoja amzoee mwenzake na ndio ukawa mwanzo wa kuanzishwa kwa jumuiya hiyo.

Rais huyo mstaafu alisema amani na utulivu ni tunu muhimu kwa taifa, hivyo viongozi wa dini hasa kupitia taasisi hiyo, wanapaswa kuendelea kusimamia amani, maadili na utulivu na kusaidia utatuzi wa migogoro mbalimbali ikiwamo ya wakulima na wafugaji. Pamoja na kutoa rai hiyo, Kikwete alionesha furaha yake kwamba hivi sasa migogoro hiyo imepungua tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo mwaka 2015.

Wahenga wanasema uzee ni dawa na ndivyo ilivyoonekana kwa Rais Mstaafu Kikwete alipozungumza kuhusu umuhimu wa kulinda na kudumisha amani, upendo umoja na mshikamano ambavyo vimetamalaki nchini.

Kwa maneno mengine, Mzee Kikwete amewakumbusha Watanzania kuwa amani si kitu cha kuchezea na pindi ikitoweka ni vigumu kuirejesha. Mfano wa hilo ni katika baadhi ya nchi ambazo wanaitafuta amani baada ya machafuko yaliyoacha maafa na majeraha miongoni mwa wananchi.

Ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania wanaishi kwa amani na upendo bila kujali itikadi zao wala imani kwa kuwa ni wamoja na wanashirikiana katika masuala yote ya kijamii na katika shida na raha. Kwa hiyo mtu yeyote anayetangaza au kushabikia udini anakuwa si Mtanzania na nia yake si njema kwa jamii nzima na taifa kwa ujumla.


Kama alivyosema Rais mstaafu, watu wanaochochea uvunjifu wa amani kwa kutumia mwamvuli wa dini wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa kuwa hawana nia njema na taifa la Tanzania.

Kwa hali ilivyo sasa, dini si kigezo cha kuwagawa Watanzania kwa kuwa Waislamu na Wakristo wana historia ndefu iliyoota mizizi kwa kuwa wameoleana au hata katika baadhi ya koo, kuna watu wa imani zote hizo mbili. Hata wale wa madhehebu ya Ahmadia, Suni na Shia kwa Waislamu, wanashirikiana katika mambo yote na wanamwamini Allah ambaye ni Mungu. Jambo la kujiuliza wafarakane kwa sababu gani.

Wakristo nao kama ilivyo kwa Waislamu wamegawanyika katika madhehebu mbalimbali na wote wanamwamini Mungu mmoja. Pia wanaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na ndiye atakayewahukumu wote siku ya kiama. Kama alivyosema Mzee Kikwete dini isitumike kuwagawa Watanzania na kusababisha uvunjifu wa amani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# CHADEMA mmemchagua Lissu, vunjeni makundi

Na Sabato Kasika

**KWA** kawaida wakati wa uchaguzi wa viongozi ndani ya chama, uchaguzi huwagawa watu kimakundi kutokana na mapenzi yao kwa mgombea fulani, huku wengine wakiwa kwa mwingine.

Mtindo huo ndio unasababisha kuwapo kwa kampeni za waziwazi au za siri ili mradi kila upande ukitamani mgombea wanayemtaka aweze kushinda, kitendo ambacho husababisha kuwapo kwa makundi.

Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa CHADEMA katika mchakato wa kumpata mwenyekiti wa chama taifa baada ya kuwapo kwa mnyukano mkali kati ya miamba miwili ambayo ni Freeman Mbowe na Tundu Lissu.

Watanzania walishuhudia mnyukano wa miamba uliosababisha hata wanachama wa chama hicho, kugawanyika na kuzusha malumbano makali kwenye mitandao ya jamii.

Hilo kimsingi ni jambo la kawaida kutokana na kwamba kila upande huwa unatamani mgombea wao ashinde, hivyo hufikia hata kufanyiana siasa za majitaka ili mradi lengo lao litimie.

Yote hayo yamepita na tayari chama kimepata viongozi wapya, kilichobaki sasa ni wanachama kutambua kuwa mchakato umeisha

kilichobaki sasa ni kuungana kuendeleza siasa za upinzani.

Jambo la kuzingatia ni kwamba katika mashindano yoyote, huwa kuna mshindi na anayeshindwa, hata ikitokea kura zimelingana, lazima mchakato urudiwe hadi mshindi apatikane.

Kwa kuwa washindi wa uchaguzi huo wameshapatikana, ninadhani haina haja kwa viongozi walioshinda kutowapenda wale ambao walikuwa upande mwingine bali watambue siasa ndivyo ilivyo.

Vilevile, waliokuwa upande ulioshindwa, wasijione kama wako nje ya chama, bali watambue kuwa uongozi ni kupokezana vijiti. Uongozi uliokuwepo kwa miaka 20 umemaliza muda wake.

Ikumbukwe kuwa chama chenu kina kaulimbiu ya "NO HATE, NO FEAR, NO FEAR NO HATE, kwa maana kwamba hamna chuki na wala woga katika kusimamia mnayoyaamini.

Ni vyema msiruhusu makundi bali muungane na kusimamia kwa pamoja mnayoyaamini kwa maslahi ya chama chenu, vinginevyo mnaweza kuyumbisha chama kikatoweka kwenye anga za siasa.

Mara nyingi makundi yanayotofautiana ndani ya vyama huwa yanavidhoofisha, vyama hivyo kwa kuwa tayari uchaguzi umefanyika, washindi wamepatikana, basi ni wakati wa kuungana.

Mwaka huu ni wa uchaguzi mkuu, ili chama kuweza kupenya katika uchaguzi huo, ni wanachama na viongozi wao kuwa wamoja na kupanga mikakati ya ushindi, kwa kutambua kuwa umoja ni nguvu.

Walioshinda uchaguzi ndani ya CHADEMA, hongera zenu na wale ambao kura hazikutosha, wasikate tamaa bali wajiandae kwa uchaguzi mwingine baada ya miaka mitano ijayo.

Kilichobaki ni kuweka nguvu za pamoja kujiandaa kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani ili kupata wawakilishi kwenye vyombo vya maamuzi kuanzia baraza la madiwani hadi bunge.

Kaulimbiu yenu iendelee kufanya kazi kwa kuepusha kuwa huyu ni wa Lissu, yule ni wa Mbowe, badala yake iwe kwamba wote ni wanachama wa CHADEMA chama kinachojitanabaisha kuwa kinajali demokrasia.

Lakini ni vyema kutambua kuwa kimantiki, makundi wakati wa kampeni ndani ya vyama huwa hayaepukiki, uchaguzi umefanyika, viongozi wamepatikana na sasa ni muda sahihi kuvunja makundi hayo.

Makundi ndani ya chama yavunjwe ili mshirikiane kwa pamoja kuweka mikakati ya uchaguzi mkuu kwani bila maandalizi chama kinaweza kuambulia sifuri kwa kuendekeza makundi.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Dada mkubwa, usiruhusu hili kujitokeza tena



Pascal Mayalla

**DEAR Dada,**

KIAFRIKA kwa vile wewe ni dada mkubwa, nakuamkia Shikamoo Dada Mkubwa!

Mimi mdogo wako, nilibahatika kuwapo Dodoma kwenye ule Mkutano Mkuu na kushuhudia kilichofanyika, hivyo kwanza niungane na Watanzania wengine wote kukuhakikishia tuna imani kubwa sana na wewe. Hatuna shaka na uwezo wako kuendelea, hivyo nijiunge na wengine wote kukupongeza ulivyoaminiwa hadi watu kuhamanika na kukupitisha kwa kishindo.

Kwa sababu kilichofanyika kimefanyika kwa nia njema, pokea pongezi zangu za dhati na pia pokea ushauri wangu japo si lazima kuufuata au kutekeleza.

Kitaaluma, mdogo wako mimi ni mwandishi wa habari na mtangazaji wa kujitegemea kwa kujitolea na pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea pia kwa kujitolea.

Sasa tuje kwenye kilichofanyika Dodoma. Ibara ya 4 ya Katiba ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inasema

Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba binadamu wote ni sawa. Kwa mantiki hiyo,

wana CCM wote ni sawa mbele ya chama.

Ibara ya 7 inasema raia yeyote wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18, anaweza kuwa mwanachama wa CCM.

Hii maana yake CCM ni chama cha wote.

Ibara ya 14, inazungumzia haki za wanachama ikiwamo ya kuomba kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa CCM na ya kuchagua viongozi wake wa CCM kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na taratibu za CCM.

Kwa ibara hiyo inamaanisha ule utaratibu wa mserereko ni batili, unaofifisha haki za wanachama kugombea nafasi za juu za uongozi, na haupo mahali popote kikatiba ndani ya katiba ya CCM.

Kwa vile wewe uliingia kwa kudra tu za Mwenyezi Mungu, bila kusailiwa, na hii ni awamu yako ya kwanza, awamu yako ya pili ya 2025-2030 unapaswa kuendelea kwa mserereko.

Dhima ya mserereko ni kuepuka 'duplicity' kwa rais ambaye amekwishasailiwa, hivyo wewe hapo mwanzo hukusailiwa na kutokana na utendaji wako wa viwango vya juu, wana CCM katika umoja wetu kupitia Mkutano Mkuu, kwa kauli moja tumeamua ni wewe tu na tumekupitisha bila kujaza fomu, bila kusailiwa na bila kupigiwa kura.

Japo kwa mujibu wa Ibara ya 100 (2)ya katiba ya CCM, Mkutano Mkuu una mamlaka yote ya kufanya jambo lolote, Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utakuwa ndicho kikao kikuu cha CCM kupita vyote na ndicho kitakachokuwa na madaraka ya mwisho.

Lakini kama hilo jambo limewekewa kanuni na utaratibu wa jinsi ya kufanyika, utaratibu ni huu kwamba Ibara ya 101 (4) inauruhusu Mkutano Mkuu, kubadili sehemu yoyote ya Katiba ya CCM kwa uamuzi wa theluthi mbili za wajumbe walio na haki ya kupiga kura kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar.

Mfano halisi ni mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzanian (JMT), lazima ajaze fomu kuomba, ajadiliwe na sekretarieti, apendekezwe na Kamati Kuu, ateuliwe na Halmashauri Kuu ya Taifa na kuchaguliwa kwa kura na Mkutano Mkuu. Mkutano huo mkuu hauna mamlaka ya kufanya vinginevyo, mpaka kwanza kutengua vifungu hivyo vilivyomo kisha kulipitisha jambo hilo lifanywe vinginevyo.

Pale Dodoma, hakukuwapo azimio lolote la kutengua kwanza kifungu chochote cha katiba, taratibu na kanuni, kwa mujibu wa ibara ya 101 (4) ndipo azimio la kumpitisha kwa utaratibu mpya likapitishwa. Pia sikuona kura za theluthi mbili za Bara na Zanzibar zikipigwa kutengua kanuni

Kutokana na hali hiyo nashauri kama ifuatavyo kwa wakati ujao;-

Mosi, katiba ya nchi ndiyo sheria mama ya nchi, hivyo katiba zote za vyama lazima zifuate sheria mama. Ule utaratibu wa mserereko wa CCM, Dada Mkubwa, naomba uondoe.

Pili, kutokana na kazi kubwa, nzuri na iliyotukuka uliyoifanya katika awamu yako ya kwanza, naamini hakuna mwana CCM yeyote atakayethubutu kujitokeza kukupinga.

Tatu, siku zote nimekuwa nikiwasisitiza wapinzani kujifunza kutoka CCM, lakini leo nashauri hakuna ubaya hata chama changu CCM kujifunza kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuhusu uchaguzi wa demokrasia ndani ya chama kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Chama.

Nahitimisha kwa ule utangulizi kukuhakikishia Dada Mkubwa kuwa Watanzania tunakupenda sana tu na tunakukubali sana. Kama ni wewe, uliyetueliwa na YEYE kuendelea 2025 -2030, ni wewe tu na hakuna mwingine yeyote zaidi yako.

Usiruhusu ule jambo lililofanyika kwenye katiba ya nchi kufifisha haki kuu ya kuchagua na kuchaguliwa, ukaingizwa ndani ya chama chetu cha haki. Usiwasikilize wahafidhina, wewe shikilia kufuata katiba ya CCM na katiba ya nchi kwa kuruhusu haki kutendeka, utabarikiwa sana.

**Nakutakia kazi njema**

**Mungu mbariki Dada Mkubwa Mungu Ibariki CCM itende Haki.**

**Mungu Ibariki Tanzania. Kaka yako mdogo Paskali.**

**KONA YA AFYA**

# Fahamu ugonjwa wa figo na namna ya kujikinga



Na Dk. Mabula Budodi

UGONJWA wa figo huanza figo zinapoanza kushindwa kufanya kazi yake ya siku zote kama awali, yaani kuchuja damu ili kuondoa uchafu ulioko mwilini au chumvi na maji yaliyozidi mwilini.

Kwa hatua ya awali, figo zinapoanza kushindwa kufanya kazi, mtu anaweza asigundue kwa haraka kwa kuwa huweza kuongeza ufanyaji kazi wa figo moja zaidi ili kupata kiwango kile kile cha ufanyaji kazi wa siku zote.

Tatizo huweza kuonekana pale tu figo zote zikiwa zimepata changamoto, yaani zimeanza kuharibika na kushindwa kufanya kazi kiufasaha. Binadamu anahitaji figo moja tu kuondoa taka mwili vizuri, hivyo kuna watu duniani wanaoishi na figo moja na maisha yanaendelea kama kawaida.

Mtu anaweza kugundulika kama mwenye matatizo ya figo ya muda mrefu au yasiyobadilika kama ufanisi wa ufanyaji figo wake umegundulika kuanza ndani ya miezi mitatu mfululizo.

**CHANZO FIGO KUHARIBIKA**

Kuna sababu nyingi zinazoweza kufanya figo kuharibika lakini sababu kuu zilizoonekana kuleta madhara ya figo zaidi ni kwa wagonjwa wa kisukari na shinikizo la damu. Zingine ni matumizi ya dawa za maumivu kwa muda mrefu

Dalili zinazoweza kuashiria kushindwa kwa figo kufanya kazi, kwanza ni figo zinapoanza kuharibika kunaweza kusiwe na dalili yoyote ambayo inaweza kuonesha moja kwa moja mpaka pale hali ya ufanyaji kazi wa figo utakapopungua kabisa.

Dalili kadhaa zinaweza kuonekana kama vile kuvimba miguu na mwili kwa ujumla, kukojoa mara kwa mara hasa nyakati za usiku, kubadilika kwa rangi ya mkojo na kuwa wa njano sana, kuwashwa mwili mzima, kuchoka sana, kukosa hamu ya kula, kutapika mara kwa mara, kukojoa damu au kukojoa mkojo wenye povu jingi na hata kuongezeka kwa shinikizo la damu maradufu.

Namna pekee inayoweza kusaidia kugundua kama tayari mtu ana matatizo ya figo au zimeharibika ni kwa kufanya vipimo vya damu ili kuangalia vichochezi vinavyopatikana kwenye damu kutokea kwenye figo ambavyo havipaswi kuwa kwenye damu. Kwa hali ya kawaida ni kupima mkojo kuangalia kama una damu au protini/kufanya picha ya tumbo au kuchukua nyama ya figo kuangalia kama zimeharibika.

**INAWEZA KUZUILIKA**

Kama mtu ana shida ya figo, anaweza kufanya mambo kadhaa kwa ajili ya kuzuia kuendelea kuharibika kama vile;-

- Kunywa dawa vizuri bila kuacha na kufuata ushauri wa daktari.
- Kuacha kuvuta sigara, kunywa pombe, kupunguza uzito kama mtu ana uzito mkubwa, kuzuia shinikizo la damu na sukari mwilini.
- Kubadili mfumo wa chakula kama inavyoshauriwa na daktari.

Kuna aina mbalimbali za matibabu zinazoweza kufanyika kwa watu wenye matatizo ya figo. Matibabu ya figo hutegemea kiwango gani cha uharibifu wa figo umefikia.

Kama bado figo zina uwezo wa kufanya kazi au uwezo wake umepungua kabisa au zimeshidwa kufanya kazi kabisa, matibabu yanaweza kuhusisha matumizi ya dawa ya shinikizo la damu au sukari, usafishaji wa figo kwa kutumia mashine, yaani kitalaamu 'dialysis' na hata kufanya upandikizaji wa figo.

**VYAKULA VYA MGONJWA WA FIGO**

Watu wenye matatizo ya figo, wanahitaji uchaguzi wa vyakula ambao utazuia kuongezeka kwa taka mwili zaidi, hivyo kuzipa kazi zaidi ambazo haziwezi kuifanya kama awali au zinafanya kwa kupungua kiwango.

Hata hivyo, aina ya ulaji wa vyakula kwa watu wenye changamoto ya figo, hutegemea hali ya afya na uharibifu wa figo wa namna gani. Hakuna chakula kimoja kilichochaguliwa kuwa bora zaidi ya kingine.

Ulaji huu hutakiwa kuhusisha kuzuia au kuacha matumizi ya chumvi nyingi kwenye chakula ambayo huweza kusababisha kuongezeka kwa shinikizo la damu zaidi na hata kunywa maji mengi sana kupitiliza kiwango kinachotakiwa.

Kupunguza kula vyakula vya protini kwa wingi kunaweza kusababusha kuongezeka kwa taka mwili zinazozalishwa baada ya umeng'enyaji wa protini hiyo mwilini.

Kupunguza kula vyakula vyenye potasiamu huweza kusababisha kuongezeka maradufu kwa potasiamu hiyo na kushindwa kutoka kwa sababu ya figo kushidwa kufanya kazi humalizikia kuleta madhara kwenye moyo.

Zaidi ya hayo, mtu anashauriwa kuonana na wataalamu wa lishe au daktari amsaidie kujua ni aina gani ya makundi ya vyakula yenye potasiamu nyingi ya kuepuka na yapi hufaa kuliwa yenye potasium inayotakiwa.

- **Dk. Budodi ni daktari wa binadamu anayeishi na kufanya kazi Dar es Salaam. Kwa ushauri na matibabu anapatikana kwa Sinu 0710 980096 au baruapepe: mabulabudodi@gmail.com**

# Serikali yasisitiza kukua utalii hifadhi za taifa

**Na Ibrahim Joseph,** MOROGORO

SERIKALI imetaja mambo manane ya maendeleo yaliyotekelezwa na kusisitiza kwamba, utalii kwenye Hifadhi za Taifa umeendelea kukua na mapato kuongezeka.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, akizungumza jana katika mkutano wake na waandishi wa Habari uliofanyika Hifadhi ya Mikumi, mkoani hapa, alisema takwimu zinaonesha mwaka 2023/24, watalii 1,863,108 walitembelea Hifadhi za Taifa.

Msigwa alisema idadi hiyo imeongezeka ikilinganishwa na watalii 1,618,538 waliotembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2022/23 ambalo ni ongezeko la watalii 244,570, sawa na asilimia 15.1.

Kuhusu maendeleo ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), alisisitiza kwamba linatekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati na mingine imefikia hatua ya kuanza kutoa huduma kwa wananchi na kuonesha mafanikio.

Msigwa alisema hadi mwisho wa mwezi Desemba, 2024 mapato yalifikia Sh. bilioni 37.6.

Kwa upande wa Maendeleo ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) alisema mpaka sasa shirika limefikisha ndege 16 na limeongeza safari za ndani ya nchi na kimataifa kwa kufikia 25.

Alisema serikali imeendelea kuweka kwenye miundombinu ya anga na kuboresha mifumo katika viwanja vya ndege vya Arusha, Kahama, Mpanda, na Songwe.

Msigwa alisema mwaka 2026 wanatarajia kukamilisha viwanja vya ndege vya Iringa, Mtwara, Songea, Kigoma, Msalato, Musoma, Shinyanga na Sumbawanga.

Katika mkutano huo pia, alizungumzia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato nchini katika sekta ya mawasiliano, huduma ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika.

Alitaja maandalizi ya uenyeji wa michuano ya CHAN 2025, AFCON 2027 na kupanda kwa ubora wa Ligi Kuu ya Tanzania.



Mchumi kutoka Wizara ya Fedha, Renatus Lucas (kushoto), akitoa ufafanuzi kuhusu akiba, baada ya kuhitimisha programu ya kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WF**

## Ujio kiongozi wa Libya kuongeza uwekezaji nchini

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Baraza la Urais la Libya, Mohamed Menfi, anatarajia kufanya ziara nchini akiongozana na ujumbe mahsusi na maofisa wa ngazi za juu katika mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika kuhusu nishati.

Mkutano huo ambao unahusu nishati unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa Habari, mmoja wa wafanyabiashara katika sekta ya madini kutoka Libya waishio Tanzania, Mohamed Abubakar, alisema ujio wa Rais huyo na msafara wake, utafungua milango kwa wawekezaji wengi kutoka Libya.

Kwa mujibu wa Abubakar, ujio huo utaongeza fursa kwa Watanzania kuungana na wafanyabiashara wa Libya katika nyanja mbalimbali za uwekezaji.

Alisema miongoni mwa watakaoambatana katika msafara huo ni Waziri wa Fedha na Waziri wa Nishati wa nchi ya Libya.

"Lengo likiwa kuingia makubaliano katika nyanja mbalimbali zikiwamo sekta za elimu, uchumi na biashara. Pia baadhi ya mikataba itatiwa saini katika ziara hii," alisema.

Alisema katika sekta ya uchumi na biashara moja ya benki nchini Libya itaingia makubaliano ya kufungua tawi lake Tanzania.

Alisema Libya inatarajiwa kuimarisha uhusiano wa kiimani (kidini) katika kuhakikisha wanasaidia taasisi za Kiislamu zinazotoa misaada ya kijamii na kusaidia vituo mbalimbali vya kulea watoto wenye mahitaji maalumu.

Machi, mwaka jana, Balozi wa Libya nchini, Abdelmajed Shetawia, alipopeleka hati za utambulisho kwa Rais Samia Suluhu Hassan, alizungumzia suala hilo.

# Wana VICOBA washauriwa kujisajili kisheria

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

SERIKALI imetoa rai kwa wananchi kuhakikisha vikundi vya huduma ndogo vya fedha vinavyojulikana kama VICOBA vinasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2028.

Kwa kufanya hivyo, watawezeshwa kujikwamua kiuchumi, kupata mikopo katika taasisi za fedha na kuondokana na changamoto za kiutendaji.

Rai hiyo ilitolewa na Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, wakati timu ya maofisa kutoka Wizara ya Fedha iliyoambatana na maofisa kutoka taasisi za Wizara ya Fedha na watoa huduma za fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha utumiaji wa huduma za fedha zilizo rasmi katika ukumbi wa Ofisi ya Tarafa ya Mbulumbulu, wilayani hapa.

Kibakaya alisema vikundi vya huduma ndogo za fedha vinavyotumiwa na wananchi katika maeneo mengi mjini na vijijini ni muhimu kusajili ili kuweza kutambulika kisheria na kupata fursa mbalimbali katika halmashauri na taasisi za fedha.

"Usajili wa vikundi vya huduma ndogo za fedha ni muhimu sana na unafanyika kwa njia ya mfumo. Mwana kikundi anaweza kujisajili bila kwenda ofisi ya halmashauri. Mfumo unaotumika unaitwa "WEZESHA PORTAL" pia halmashauri zote nchini wako waratibu wa huduma ndogo za fedha ambao watawasaidii kupitia mfumo huo" alisema.

Kibakaya alisisitiza kuwa usajili wa vikundi vya huduma ndogo za fedha utawawezesha pia kunufaika na mikopo ya halmashauri ya asilimia kumi inayotolewa na Serikali ambayo imeanza kutolewa ili kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Ofisa Sheria Mwandamizi kutoka Kurugenzi ya Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ramadhani Myonga, alisisitiza wananchi kusoma mikataba ya mikopo ili kujua masharti ya mikataba na utekelezaji wake na kuwa wa uhakika wa urejeshaji wa mkopo ili kuepuka migogoro na watoa huduma.

Aidha, alisisitiza wananchi kuzingatia kiwango cha mkopo wanachopokea kilingane na kiwango kilichoandikwa katika mkataba, kufahamu riba ya mkopo, aina ya urejeshaji na kufahamu adhabu ya kuchelewesha kurejesha mkopo kabla ya kusaini mkataba.

'Ni muhimu kuhakikisha mkataba una kipengele kinachotoa fursa ya majadiliano juu ya marekebisho ya masharti ya mkataba ikiwemo kuongezewa muda wa marejesho ili kumpatia nafuu ya marejesho tofauti na awali endapo mkopaji atapata changamoto itakayosababisha kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati,' alisisitiza Myonga.

Mratibu wa Huduma Ndogo za Fedha Wilaya ya Karatu, Joshua Mwamsojo, alisema mafunzo hayo yatawezesha wananchi kufuata Sheria na taratibu za namna ya ukopaji, ili kuepukana na mikopo isiyo rasmi.

"Naipongeza serikali kwa mafunzo haya na nitoe rai mafunzo haya yawe endelevu ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na kusaidia kuondokana na changamoto za fedha.

"Natoa wito kwa wananchi wa wilaya ya Karatu waepuke kukopa katika taasisi zisizo rasmi, watumie elimu waliyoipata katika kupanga matumizi ya fedha wanazopata na nina Imani yatawasaidia kujikwamua kiuchumi dhidi ya umaskini," alisisitiza.

Maeneo yaliyofikiwa katika wilaya ya Karatu ni pamoja na Kata ya Karatu Mjini, Tarafa ya Endabash (Kata za Kansay, Buger na Endabash), Tarafa ya Eyasi (Kata za Mang'ola na Baray) na Tarafa ya Mbulumbulu (Kata za Rhotia na Mbulumbulu).

Baada ya kuhitimisha programu , timu hiyo ya wataalam inaendelea na programu katika wilaya za Ngorongoro na Longido.

MAIS
JANUARI 26, 2025
Nipashe




# JAZA NYWELE ZAKO
## Kwa parachichi, yai, asali

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | M | A | M | B | O |
| C | | | | W | | N |
| H | | B | A | I | | D |
| A | D | A | | Z | A | O |
| N | | M | E | I | | L |
| G | | I | | | | E |
| A | M | A | N | A | | A |


## FUMBO TOTO

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


MTO, TIA, NAO, ARA, NGANO, AGANA, AGANO, TAMBA, ONGOPEA, MAJANGA



## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

TUMSAIDIE MAMA KUKU KUKIFIKIA KIFARANGA CHAKE!



## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Vijue vifutio vya ndoto unazoota usiku

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu kufutwa au kuchafuliwa kwa ndoto zetu tunazoota usiku tumelala.

Kumbuka ndoto unayoota inahusiana sana na mipango yako. Ni kitu halisi kinachoanzia kwenye ulimwengu wa roho. Mungu huongea na sisi sana kupitia ndoto ili kuifanya hiyo ndoto iwe wazi.

Ndoto ni mjumbe anayekuletea habari ya kile kinachoendelea kwenye ulimwengu wa roho, ule usioonekana kwa macho ya damu na nyama. Yaani ukoje wewe katika ulimwengu wa roho.

Ndoto ni kile ambacho Mungu amekupa kukifanya duniani. Lakini adui hufuta na kuzichafua ndoto zako ili usifanikiwe katika maisha yako.

Mungu husema nasi katika ndoto. Na katika maandiko yake amesema na watu mbalimbali wakiwemo manabii. Kwa mfano aliwaambia Haruni na Miriamu, “Sikilizeni basi maneno yangu; Akiwapo nabii kati yenu, Mimi BWANA nitajifunua kwake katika maono, Nitasema naye katika ndoto. Hesabu 12:6).

Hebu sasa tuende zaidi tuangalie ndoto zetu zilizochafuliwa, zinafutwaje kwenye ulimwengu wa roho? Cha kwanza unapoota ndoto unalishwa chakula. Hicho kinaitwa ni chakula kichafu kilichochafuliwa.

Unapoota ndoto unalishwa chakula hiyo ni kifutio cha ndoto. Mara nyingi watu wengi wanaoota kula vyakula kwenye ndoto inakuwa ni vyanzo vya kufuta ndoto zako zilizo wazi.

Hata ukiota ndoto ya kitu kizuri, Mungu anakuonya jambo fulani huwezi kuelewa chochote, ukiamka asubuhi umesahau. Lakini utagundua uliota ndoto ya kula chakula ndotoni.

Hiyo inakuwa ndoto zako zimechafuliwa. Ni ujumbe ambao umechafuliwa. Ni sawa na umeletewa barua lakini juu ya hiyo barua mtu akaandika vitu vyake vingine akaichafua.

Unaota ndoto mwanzoni kilikuwa ni kitu kizuri kisha mwishoni kitu kinatokea kama vile amekula chakula na vyote vizuri vinafutika. Na hii haitokei tu katika kusahau ndoto bali hata kusahau mambo ya ibada nyumba za dini.

Mtu anaingia kwenye ibada anasikiliza vizuri mafundisho ya Mungu na yanamgusa, lakini akitoka hapo, maadui wameshafuta. Hapo kuna mtandao wa vyakula vya kichawi ulivyokula ndotoni unafuta. Mapepo na chachawi, hawa ndio wahudumu wazuri wa kuchafua kabisa ndoto au kuzifuta.

Futio mojawapo ni kulishwa vyakula kwenye ndoto. Ukishalishwa chakula, tayari mfumo wa kufuta vile vitu vizuri unafuta. Wewe utakachokumbuka ni ndoto ya kula chakula.

Kumbe adui ameshajua kuwa huyu mtu anataka atambue siri fulani ambayo Mungu anasema naye kupitia ndoto. Adui analeta hiyo unashangaa amefuta.

Kifutio kingine cha pili cha ndoto ni ndoto za vitisho. Yaani unatishwa kwenye ndoto. Inawezekana ukawa na ndoto njema kabisa ambayo inakutahadharisha jambo, lakini hizi zingine zimetokea za vitisho unashtuka unaamka. Unashangaa zile ndoto ulizoota zote zimefutika!

Lakini adui alitumia mbinu ya kukutisha kwenye ndoto. Mungu anakupa ujumbe mzuri lakini adui analeta picha ya kukutisha, anafuta ndoto nyingine zote nzuri za hatma yako.

Unaamka unakumbuka ni kama vile ulikuwa unakabwa usiku, unakimbizwa na watu usiowajua. Kumbe hapo ni adui alikuja kukutisha ili kufuta ule ujumbe wa Mungu wa ndoto zako njema!

Na hujui cha kufanya, wewe unajua tu ulikimbizwa kwenye ndoto, utaanza kukemea majinamizi, unaishia hapo. Kumbe kuna mbinu iliyotumika ya kufuta ujumbe kamili ambao Mungu alikuwa anakupa kwenye ndoto.

Kifutio cha tatu, ni kuota ndoto unafanya zinaa yaani, unazini kwenye ndoto. Anatumika mwanamke wa kichawi au mwanaume wa kichawi. Unakuta umefikia kitu cha upenyo mzuri adui analeta kifutio cha ndoto hiyo mbaya.

Unashangaa alfajiri uliishia kufanya mapenzi kwenye ndoto. Unajiuliza, mbona kuna kitu nilikipata kwenye njozi halafu alfajiri naanza kuota ndoto za ajabu ajabu ndio nashtuka? Unasema naikumbuka ile ya mwisho ya zinaa kwenye ndoto.

Hicho ni kifutio, adui ametumia ile picha ya mwisho kufuta ndoto nzuri. Ni sawa na mtu umepata ujumbe wako mzuri, unatoka pale umechangamka, unakutana na vitu njiani vinakufutia kila kitu.

Hizo ndoto ungezikumbuka ujasiri ungeongezeka ndani yako. Ila unazokumbuka ni za kubakwa na kadhalika. Ndoto nyingi ambazo Mungu alikuletea zimefutwa. Mjue sana Mungu upate maarifa kufuta ndoto mbaya!

**Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kuhusu yale yanayojiri kwenye ndoto usiku. Hadi wiki ijayo. Una maoni? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Hili la kuunda tume ya upatanisho CHADEMA lisipuuzwe

AJENDA kuu ya Mwenyekiti mstaafu wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kabla ya kushindwa katika uchaguzi wa chama hicho, uliofanyika Januari 21, mwaka huu, ilikuwa kuunda Tume ya Ukweli na Upatanisho endapo angeshinda.

Mbowe angeunda tume hiyo kwa shabaha moja tu, kutibu majeraha ya uchaguzi huo uliokuwa na tashtiti nyingi, kuvuana nguo, kejeli na kudharauliana wanasiasa na wapambe wao. Alitaka kuhakikisha CHADEMA yote inarudi katika umoja na mshikamano, chini ya kaulimbiu yao ya ‘Stronger Together’.

Kwa kuzingatia hilo, Tundu Lissu, Mwenyekiti mpya wa CHADEMA, amebebeshwa kazi ya kuyaleta pamoja makundi mawili yanayohasimiana hadi sasa,licha ya uchaguzi kumalizika.

Wako wanaolalamika mitandaoni, kutumiwa ujumbe wa vitisho vya kufutwa uanachama na tawi, baada ya kundi mojawapo kushindwa. Tusifike huko kama kweli ninyi ni wana mabadiliko na waumini wa haki na demokrasia.

Mpasuko ndani ya chama siku zote hudhoofisha chama chochote kile kinachosaka wafuasi wengi wa kukipigia kura na kupata ushindi katika chaguzi ili kushika dola.

Lissu alishinda kwa kura 513 (sawa na asilimia 51.5), dhidi ya Freeman Mbowe, aliyepata kura 482 (sawa na asilimia 48.3. Hii ni baada ya miaka takribani 20 ya uongozi wa Freeman Mbowe, aliyechukua hatamu za kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA tangu 2003.

Hata mpinzani wake katika uchaguzi huu, Tundu Lissu, amekiri kukua kwa CHADEMA kunatokana na kazi kubwa iliyofanywa na Mbowe.

Bila shaka, ni jambo la kushukuru kwa wafuasi wa CHADEMA kwamba kamera za vyombo vya habari hazijanasa matukio ya watu wakishika vikosi katika uchaguzi huu; kwa jinsi ushindani, malumbano na maneno yalivyokuwa mengi.

Freeman Mbowe amekubali kushindwa na kumpongeza Lissu, hicho peke yake ni kiashiria cha ukomavu wa kisiasa.

Hakuna ubishi, Lissu ameshika nyadhifa nying; zikiwemo Mbunge wa Singida Mashariki, Mwanasheria Mkuu wa CHADEMA, Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Makamu Mwenyekiti-Bara, na sasa ni mwenyekiti mpya wa taifa.

Kama ilivyo kwa ushindi wowote; furaha hutamalaki. Swali la kujiuliza ni je, Lissu ataifanyia nini CHADEMA au CHADEMA itamfanyia nini? Uso wake, hisia zake na uanaharakati wake, utamsaidiaje kukabiliana na changamoto zijazo na zile ambazo tayari ziko mbele yake?

Je, ataweza kuboresha, kutanua na kuendeleza utekelezaji wa programu muhimu za ujenzi na ustawi wa chama chake na wanachama (on-going programs)?

Yako mengi yanayomsubiri, kama kuamsha vuguvugu kali la madai ya Katiba Mpya, Tume Huru ya Uchaguzi, na sheria za uchaguzi, kwa kutumia nguvu ya umma. Matahalani, vitu kama kuanzisha programu kabambe na endelevu ya kuandaa na kuwawezesha wagombea wa CHADEMA kushinda chaguzi.

Anapaswa kwenda mbali zaidi kufuta minong'ono kwamba kichwa cha Mbowe ndicho kilikuwa ‘custodian’ na injini ya kusaka fedha za chama.

Mambo hayo na jitihada nyingi za kutafuta fedha zinahitajika kwake binafsi, ili kugharamia sehemu kubwa ya gharama za kampeni na ulinzi wa kura katika chaguzi zote, kuanzia urais, ubunge na udiwani.

Hakuna namna anapaswa kuanzisha programu ya kimkakati na endelevu ya kutoa elimu ya uraia na elimu ya siasa, ili kutengeneza jamii kubwa ya Watanzania wenye uelewa mkubwa na ujasiri wa kutosha katika kupigania haki zao za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Januari 17, mwaka huu, wakati akizungumza katika mdahalo wa kisiasa, Lissu alinukuliwa akisema: “Mimi ndiye niliyekuwa wa kwanza kupuliza filimbi kwamba kuna rushwa kwenye chaguzi zetu (CHADEMA).

“Tuna tatizo. Muda huu tunapozungumza, kuna wajumbe wanasafirishwa, wanawekwa kwenye mahoteli, makambi, wanapewa pesa, wanalishwa na wagombea. Kuna uchafuzi wa aina hiyo, unoafanywa na wagombea na wapambe wao.”

Hili ni tatizo ambalo wakati fulani huko nyuma lilizungumzwa pia. Mwezi Mei mwaka 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), ilitangaza kuanzisha uchunguzi kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha ndani ya CHADEMA. Kazi kwake!

• ***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI



Ilikuwa siku ya furaha kwa Mussa na mkewe Fetty baada ya kukubaliana kufunga ndoa hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MC GaraB**

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# MAVAZI HAYA USIYAKOSE

WANAUME ambao wanajali kuhusu kuvaa wanaelewa namna ya kuwa na aina fulani ya mavazi kwa ajili ya matembezi ya hapa na pale.

Pamoja na kuvaa mitindo tofauti maalumu ya mavazi, unatakiwa kuwa na aina za nguo ambazo zitakufanya usipate tabu kufanya chaguo sahihi.

Hizi ni aina ya nguo ambazo unatakiwa kuwa nazo nyumbani wakati wote.

**FULANA ZA PAMBA**

Fulana za pamba zinadumu kwa muda mrefu, nunua nguo hizi zilizotengenezwa kwa pamba pekee zenye rangi tofauti.

Rangi zinazopendekezwa ni nyeupe, nyeusi, rangi ya kijivu
na rangi kali kama njano, bluu nyepesi na kijani.

**FULANA ZA POLO**

Mwanaume yoyote anatakiwa kuwa na fulana za Polo zenye kola zinafaa sana kuvaliwa kazini kwenye siku za mwisho wa wiki.

**MASHATI YA KAWAIDA**

Mashati ya kawaida, ya mikono mirefu au mifupi, ni mazuri kuvaa na jeans na viatu au raba. Pia, zipo za aina na rangi tofauti kwa hiyo tafuta itakayokufaa.

**BUKTA**

Kutokana na hali ya joto, ni muhimu kuwa na bukta kwa ajili ya kuvaa ukiwa nyumbani au matembezi ya jioni.

Kuna aina nyingi za bukta na zenye rangi tofauti, zote zinapendeza kuvaa na fulana na viatu vya kawaida.

**SURUALI ZA KAWAIDA**

Suruali za aina hii zina faraja na zinavaliwa kwenye mazingira mbalimbali. Pia zinapatikana kwa rangi nyingi kwa hivyo unakuwa na uwanja mpana kufanya uchaguzi.





UREMBO

Na Mary Geofrey

# JAZA NYWELE ZAKO

## Kwa parachichi, yai, asali

UREMBO kwa mwanamke ni jambo la msingi sana ambao unatakiwa kuzingatiwa wakati wote.

Ili uendelee kuwa mrembo unapaswa kujifunza kwa waliofanikiwa.

Kuwa mrembo ni sifa inayompamba mwanamke kwa kiwango kikubwa.

Urembo kwa mwanamke huanzia kichwani, usoni, ngozi na mwonekano wa mtu ndio unamfanya aonekane mrembo.

Leo tutaangalia urembo wa nywele hasa namna unavyoweza kujaza nywele za kichwani kwa kutumia parachichi, kiini cha yai na asali.

**Mambo ya kuzingatia**

Chukua parachichi kubwa moja na asali vijiko vitatu na kiini cha yai.


Osha nywele zako kwa shampoo na uzikaushe.

Ponda ponda parachichi mpaka lilainike kabisa. Chukua vijiko vitatu vya asali na kiini cha yai kisha changanya yote kwa pamoja.

Paka mchanganyiko huo kaa nao kwa muda wa dakika 15 kisha osha.

Fanya hivyo kwa muda wa wiki moja hadi mbili na utaweza kuona matokeo mazuri katika nywele zako.

Nywele zako zitakuwa na mvuto na kuendelea kuongeza kunogesha urembo.











MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mishkaki ya maini na figo



MAINI na figo ni nyama inayopatikana ndani ya ng'ombe. Wengi wanapendelea kuzipika au kukaanga kwa nyanya na kuyafanya chakula pendwa kwa kila mtu.

Leo katika safu yetu ya mapishi tutaelekeza namna ya kutengeneza mishkaki ya maini na figo.

**Mahitaji**

Maini na figo robo kilo yakatwe vipande vya saizi, pilipili manga nusu kijiko cha chai, udaha (Cayenne) robo kijiko cha chai na punje tatu za kitunguu swaumu kilichosagwa na unga wa tangawizi kijiko kimoja cha chai.

Mahitaji mengine ni Soy Sauce kijiko kimoja cha chai, chumvi kiasi upendacho, mafuta ya kupikia kijiko kimoja cha mezani na stiki za mishikaki, ziloweke kwenye maji kwa dakika 30, itazuia kushika moto kwa haraka

**Jinsi ya kuandaa**

Chukua bakuli weka maini na figo kisha weka na viungo vyote. Ukiisha changanya vema wacha vikae kwa dakika 20.

Baada ya dakika 20 andaa kuweka mishikaki yako katika vijiti. Kisha anza kuchoma kwa moto usio mkali sana.

Ikiishaiva waweza tengeneza chachandu yako ukala au ukakamulia limao tu ukala.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# WEKA SAKAFU KWENYE NYUMBA INAYOENDANA NA WAKATI

KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna mbalimbali, yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya sasa.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yatakayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba. Katika nyumba, sakafu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hasa pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.





Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake.

Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, kwa mujibu wa Kashozi, ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.



# Tengeneza chumba cha maombi

Na Restuta James

WATU wengi wanajenga nyumba wanaweka vyumba vya kulala na maeneo ya kupumzika, lakini wanasahau chumba cha maombi.

Walio kwenye nyumba za kupanga, hali ni hiyo hiyo, wengi wanasahau kuwa na sehemu maalum ya kufanya maombi, eneo ambalo wanapaswa kulitenga maalum kwa ajili hiyo pekee.

Wataalamu wa ujenzi wanashauri kwamba, chumba au eneo la sala (kwa wenye nyumba ndogo), linapaswa kupewa kipaumbele kama watu wanavyowaza kuwa na choo, bafu, jiko, sebule na vyumba vya kulala.

"Ni eneo muhimu sana ambalo watu wengi wanalisahau. Hata kama kuna wakati utaongea na Mungu ukiwa kitandani, kutenga eneo maalum la kufanya sala ni muhimu kwa ajili ya kutengeneza mazingira ya utulivu," anasema Grace Josephat.

Anasema kuweka chumba au eneo mahsusi la maombi kunaongeza muda wa kufanya hivyo, kuliko kutokuwa nayo.

"Hata ukiingia kuomba, unaweza kupata muda wa kutafakari maandiko matakatifu kutokana na mpangilio wa eneo husika," anasema Grace.



**DONDOO MUHIMU**

Hata kama huna chumba kizima unachoweza kukitumia kwa maombi, tengeneza kona ya kufanya hivyo. Kama mnalala wawili chumbani, hapo sio mahali pazuri pa maombi kwa kuwa mmojawenu anaweza asiwe tayari kwa maombi, wakati mwingine anataka kuamka usiku kusali. Kama uko peke yako na huna chumba kingine, hapa ni sehemu sahihi.


Chumba cha kulala kinaweza kukupa uvivu wa kuamka kufanya maombi, ndio maana inashauriwa utenge eneo litakalokusaidia kutekeleza uamuzi wako.

Kama ni chumba kizima, paka rangi tulivu (bluu, kijivu mpauko), nyeupe au yeyote unayoona inakupa utulivu.

Weka mito michache kulingana na ukubwa wa chumba au eneo, picha nzuri ya ukutani hasa inayoonesha mazingira asilia kama msitu.

Meza ndogo ambayo utaweka vitabu pamoja na mishumaa. Unaweza kuweka maua yanayozalisha oksijeni kwa wingi, ili kukifanya chumba kuwa na hewa safi ya kutosha.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2025
SMS - 0713 447766
MSHAWAHI KUMTWISHA?
NDIO MAANA UNAAMBIWA KICHWA CHA NYOKA HAKIBEBI MZIGO!
SIO WAKATI WA KUCHIMBANA... UKIMUONA MTU KALA SUTI ALAFU HANA KWA KWENDA "PIGIA MSTARI"
JUKWAANI
HAPO KWA "KUPIGIA MSTARI" FAFANUA
HA HA HAAA!!! SASA NIME-GUNDUA KUWA DAGAA MBOGA!
MSITUYEYUSHE NA KINGEREZA CHENU KIBOVU!
KIZUNGU GANI KIMEJAA ZE' ZE ZE...OFU KOZI NYINGIIIII!!!
DEREVA HAWA WASITUCHANGANYE PAKI GARI BAR TUJIBU MAPIGO.
HAWA WATAKUWA WAMEYACHAPA MAJI, SASA KIZUNGU HEWA KINAWATOKA!
GERE YA NINI?! NA NYIE SI-MKASOME INGLISHI KOZI?
HII NGOMA SIJUI NANI ATAIONA KAMA NAICHEZA KWA MBINDE!
RIBA-MIKOPO
KADRI NINAVYO-ZUNGUSHA RAUNDI NA AKILI NDIVYO INAVYOZUNGUKA!
HUJA-TUMWA "SANDA" KWELI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...SIKIO LA MBEA HALISIKII JAMBO JEMA...

## HABARI KIMATAIFA

# Jeshi la DRC laapa kuilinda Goma kwa jasho na damu

**GOMA,** DRC

JESHI la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, limepambana kuulinda mji wa Goma dhidi ya waasi wa M23 ambao wameuzingira wakitaka kuudhibiti.

Hata hivyo, wanajeshi wa Umoja wa Mataifa nchini Congo, (MONUSCO), waliingilia kati kuwashambulia waasi hao ambao wamefika nje ya viunga vya mji huo mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini.

Taarifa kutoka MUNUSCO, ilieleza kuwa vikosi vyake vya kulinda amani, vilishiriki katika mapigano makali dhidi ya M23.

Taarifa hiyo ilisema vikosi hivyo kwa kushirikiana na jeshi la serikali vimeshiriki kikamilifu katika mapigano makali na katika muda wa zaidi ya saa 48 kwa kushambulia ngome za M23.

Umoja wa Mataifa umeonya kuwa mapigano hayo yanayoendelea katika jimbo la Kivu Kaskazini yamesababisha zaidi ya watu 400,000 kuhama makazi yao mwaka huu na huenda ukaibua vita vya kikanda.

Wakati huohuo nchi za Uingereza, Marekani na Ufaransa zimewataka raia wao kuondoka haraka katika mji wa Goma.

Katika taarifa zilizotumwa kwa njia ya mtandao au moja kwa moja kupitia barua pepe, raia wa Marekani, Uingereza na Ufaransa walihimizwa kuondoka Goma wakati viwanja vya ndege na mipaka bado haijafungwa.

Wakimbizi waongezeka

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi (UNHCR), Matthew Saltmarsh, aliwaambia waandishi wa habari mjini Geneva kwamba idadi ya waliokimbia makazi yao kufikia sasa ni zaidi ya watu 400,000 mwaka huu pekee, hii ikiwa karibu mara mbili ya idadi iliyoripotiwa wiki iliyopita.

Saltmarsh, alisema UNHCR ina wasiwasi kuhusu usalama wa raia na wakimbizi wa ndani katika eneo hilo la mashariki.

Alisema mashambulizi makubwa ya mabomu yamesababisha familia kuondoka katika kambi tisa za watu waliokimbia makazi yao viungani mwa mji wa Goma na kwenda kutafuta usalama.

**Hata hivyo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa litakutana Jumatatu kuhusiana na ghasia hizo zinazoendelea nchini DRC.**

Katika taarifa, msemaji wa katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, alisema mkuu huyo amesikitishwa na kurejea kwa uhasama kati ya pande hizo mbili.

Hata hivyo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa litakutana Jumatatu kuhusiana na ghasia hizo zinazoendelea nchini DRC.

Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, alifanya mkutano wa baraza la ulinzi hapo juzi kufuatia mkutano wa dharura wa baraza la mawaziri.

Katika hatua nyingine, jeshi la DRC limeapa kulipiza kisasi kufuatia kuuawa kwa gavana wa kijeshi wa Kivu Kaskazini, Jenerali Peter Cirimwami.

Cirimwami alipigwa risasi siku ya Alhamisi karibu na mstari wa mbele wa vita.

Vyanzo vya kijeshi vilisema mapigano yalifanyika siku nzima jana umbali wa takriban kilomita 20 magharibi mwa Goma, ambapo huduma za mitandao ya simu na intaneti pamoja na umeme zilikatizwa mara kwa mara.

**DW**

## Marekani yasitisha misaada yote duniani

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesitisha misaada yote ya kigeni kwenda sehemu yoyote Duniani, isipokuwa ile inayolenga chakula cha dharura na ufadhili wa kijeshi kwa Israel na Misri.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Marco Rubio, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa sera ya Rais Donald Trump ya kutoa kipaumbele kwa maslahi ya Marekani.

Ujumbe uliotumwa kwa wafanyakazi wa wizara hiyo, ulisema hakuna fedha zitakazotolewa kwa ufadhili mpya au kuongezwa muda kwa ufadhili uliopo, hadi kila pendekezo jipya litakapotathminiwa na kuidhinishwa upya .

Hata hivyo, Rubio aliagiza kuendelea kwa ufadhili wa Marekani kwenye misaada ya dharura ya chakula, ambayo nchi hiyo imekuwa ikichangia kufuatia machafuko duniani kote ikiwa ni pamoja na Sudan na Syria.

Mwaka 2023, Marekani ilitoa misaada ya maendeleo ya zaidi ya dola bilioni 64.



Mateka wanne raia wa Israel wakiwasalimia watu baada ya kuachiwa na kundi la Hamas mjini Gaza jana. **PICHA: REUTERS**

# Hamas yawaachia mateka wanne

**GAZA,** PALESTINA

RAIA wanne wa Israel ambao walishikiliwa mateka na kundi la Hamas, wameachiliwa jana katika kutekeleza makubaliano ya kusitisha vita.

Tofauti na makabidhiano ya mwishoni mwa wiki iliyopita, mateka hao walikabidhiwa katika hafla iliyowavutia Wapalestina wengi.

Mateka walioachiwa jana ni askari mmoja Karina Ariev, Daniella Gilboa, Naama Levy na Liri Albag.

Kuachiwa kwa matekao hao kunafanyika kwa kubadilishana na wafungwa 180 wa Kipalestina wanaoshikiliwa nchini Israel.

Wasichana hao wanne waliibuka wakiwa kwenye magari yaliyolindwa na watu wenye silaha waliojifunika nyuso zao na kuwekwa kwenye eneo lililoandaliwa, kabla ya kuchukuliwa na ofisa wa shirika la Msalaba Mwekundu ambaye alitia saini nyaraka na mpiganaji wa Hamas.

Watekaji hao walionekana wakiwa wamevalia mavazi yanayofanana huku shingoni mwao wakiwa wamening'iniza vitambulisho.

Muda wote watu wenye silaha waliojifunika nyuso zao wakiwa wamesimama karibu yao, kila mmoja akiwa na aina yake ya kibali kwa ajili ya tukio hilo.

Karibu na jukwaa kulikuwa na meza, viti, bendera na bunduki aina ya machinegun.

Huku mamia ya wapiganaji wa Hamas na raia wa Palestina wakiwatazama, mateka hao wa Israel walionekana wakitabasamu, wakishikana mikono na kusalimiana.

Hamas iliwapa kila mmoja nyaraka na mikoba ya kubebea vitu vyao.

Wiki iliyopita, watu wengi walikuwa na hasira baada ya wanawake watatu wa kwanza walioachiwa huru kuondolewa bila utaratibu maalumu.

**BBC**

# Rais Samia ataka vijana kugombea ubunge, udiwani

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesisitiza vijana kugombea ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Aliandika hayo juzi katika ukurasa wake X akitilia mkazo hoja iliyoandikwa na mtumiaji wa mtandao huo, aliyejulikana kwa jina la Thomas Kibwana akiwakumbusha vijana kushiriki uchaguzi huo.

Msisitizo huo umekuja wakati utafiti wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni wa mwaka 2022, ukionesha kuwa asilimia 40 ya vijana wenye sifa hawashiriki kwenye uchaguzi.

Akichangia hoja hiyo, Rais Samia aliwakumbusha vijana kuwa kushiriki Uchaguzi Mkuu ikiwamo kugombea nafasi za uongozi ni sehemu ya wajibu wao.

Rais Samia alisema uhuru na ulinzi wa mapinduzi ya nchi unajengwa na kuwapo kwa vijana wenye uthubutu hasa katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

"Huu ni ushauri mzuri hasa wakati huu kuelekea uchaguzi mkuu. Sehemu ya wajibu wa vijana wetu ni kushiriki mchakato wa uchaguzi, ikiwamo kugombea nafasi za uongozi na kutumikia ipasavyo wanapopata nafasi," alisema.

Hoja ya Kibwana ililenga kuwasisitiza vijana kuchukua fomu na kuwania nafasi za udiwani na ubunge bila kujali vyama wanavyoviwakilisha.

"Vijana chukueni hizo fomu mwaka huu mgombee nafasi za udiwani na ubunge. Haijalishi upo chama gani wewe chukua fomu gombea," aliandika Kibwana.

Vilevile, Rais Samia alishukuru kwa kupata nafasi ya kujifunza kwa vitendo kwa miaka mitatu katika ulingo wa siasa akisisitiza kuwa, msingi wa siasa na uongozi ni utumishi na kumtanguliza Mungu. "Ukishatanguliza hilo pamoja na kuomba mkono wa Mwenyezi Mungu, mengine yatakwenda vizuri, ikiwamo mikakati ya utekelezaji wa unayokusudia," alisema.

Aliandika hivyo akimshukuru mtumiaji wa mtandao X, AshaDi aliyemsifia kuwa ni mtaalam wa siasa na demokrasia nchini.

"Ila utani pembeni, Dk. Samia Suluhu Hassan ni mtaalamu wa siasa na masuala ya siasa," aliandika.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) mwaka 2020 ulionesha kuwa ni asilimia 64 pekee ya vijana walioshiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na ulikuwa upigaji kura, na asilimia ndogo zaidi wakijitokeza kama wagombea kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Kwenye takwimu hizo, asilimia 35 ilikuwa vijana waligombea nafasi za wenyeviti wa kijiji, nafasi za udiwani (asilimia 27) na nafasi za ndani ya vyama vyao vya kisiasa (asilimia 24), huku asilimia 14 wakihudumu kama wajumbe wa mabaraza ya serikali za mitaa.

# JKCI yatumia bil. 2/- kliniki za matibabu

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), imetumia zaidi ya Sh. bilioni mbili, kuanzisha na kuwezesha miundombinu ya kliniki mbili, ikiwamo JKCI-Oysterbay, jengo la Oester Plaza, Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliyasema hayo juzi ana, jijini Dar es Salaam mbele ya Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, wakati akizindua kliniki hiyo.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Mhagama, alisema ongezeko la kliniki za JKCI, ambazo zimefikia tatu pamoja na makao makuu ya JKCI-Upanga, limeipunguzia gharama serikali katika kusafirisha wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Alisema Tanzania imeendelea kwenye matibabu ya kibingwa na bobezi, ikiwamo kutoa fursa ya masomo hayo wekeza zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa kuboresha ujuzi wa matibabu bobezi na kibingwa kwa wataalamu wa afya wazawa.

"Kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2021, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kibingwa, wakiwamo wataalamu kutoka JKCI wapatao 47. Hii imesaidia kufanya matibabu ya kibingwa kufanyika nchini na kuokoa fedha," alisema.

Waziri Mhagama alisema matibabu ya moyo ni muhimu, ikizingatiwa kwamba mwaka 2019 Shirika la Afya Duniani (WHO), watu waliopoteza maisha kwa mwaka walikuwa milioni 17, sawa na asilimia 32 ya vifo vyote duniani.

"Uwapo wa taasisi hii unapunguza idadi ya vifo vitokanavyo na tatizo la eneo hilo nchini. Ili kuendeleza huduma hizi tunahitaji kujitangaza kwa kushirikiana na balozi za ndani na nje, wafahamu huduma zetu na itakuza tiba utalii," alisema.

> **"Kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2021, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kibingwa, wakiwamo wataalamu kutoka JKCI wapatao 47.**

Awali, Dk. Kisenge alisema taasisi hiyo imeendelea kukua na sasa ikiwa na vituo vinne vya huduma, Upanga, Kawe, Oysterbay na Dar Group, vyote vilivyoko Dar es Salaam, huku mikoa mingine ikifikiwa na tibamkoba.

"Tulipoanza huduma za matibabu ya moyo JKCI operesheni tuliofanya ilikuwa ni watu 365 kwa mwaka. Sasa zimefikia zaidi ya 3,000 kwa mwaka ikiwamo upasuaji mkubwa wa kufungua kifua.

"Zaidi ya Sh. bilioni 2.2 zimetumika katika kufungua kliniki ya Kawe na Oysterbay, kutokana na uwekezaji wa kliniki hizo mbili za JKCI, tumepanua wigo wa huduma wa matibabu na ushauri wa lishe," alisema bingwa huyo wa moyo.

Kadhalika, alisema JKCI pia katika tawi la Oysterbay itafanya ushauri wa kidaktari kwa mgonjwa kwa njia ya mtandao na kuwa rahisi kwa anayeugua kupata huduma popote alipo.

"JKCI inaendelea kujengea uwezo wataalamu wa magonjwa ya moyo nchi tofauti Afrika na tumefanya hivyo katika nchi zipatazo 20. Taasisi sasa imekua, idadi ya vitanda imeongezwa kutoka 156 na sasa ni takribani 280, ingawa bado kuna mahitaji makubwa," aliongeza.

Alisema kutakuwapo maabara ya lishe ambayo kazi yake itajikita katika kubaini kuhusu Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD) na taasisi itaendelea kwenda mbali na matarajio ni kufika kila mahali nchini.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mesenja kaleta balaa, meneja kapigwa vibao*



**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI mtunzi na mwimbaji, Maximillian Bushoke, alikuwa mmoja wa waliochukuliwa kutoka DDC Mlimani Park kwenda Orchestra Safari Sound (OSS), wakati huo ikitumia mtindo wa Ndekule, katikati ya miaka ya 1980.

Mwanamuziki huyo aliyeanzia kwenye bendi ya Vijana Jazz, hakupata umaarufu mpaka alipojiunga na DDC Mlimani Park Orchestra.

Umahiri wake kwenye utunzi, aina yake ya kutunga nyimbo pamoja na staili ya uimbaji, vilimpatia sifa kubwa. Alikuwa mmoja wa watunzi wa nyimbo nyingi kwenye bendi hiyo inayotumia mtindo ya Sikinde Ngoma ya Ukae.

Sauti yake nzito na ya kulalamika, ilianza kuwa alama ya Sikinde. Alikuwa staa zaidi, pale wanamuziki Hassan Bitchuka, Muhidini Mwalimu Gurumo na wengine walipoihama Sikinde mwaka 1985 na kujiunga na OSS, kuziba pengo la Freddie Ndala Kasheba, aliyemaliza mkataba wake mwaka 1984 na kurejea Orchestra Maquis Original. Walipofika OSS walianzisha mtindo wa Ndekule badala ya ule wa awali, Dukuduku.

Baada ya Bitchuka kurejea Sikinde mwaka 1987, Ndekule ilimchukua Bushoke ambaye alikuwa hana bendi baada ya kufukuzwa Sikinde kwa madai ya utovu wa nidhamu. Baada ya kujiunga na OSS, aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo, Gurumo alitamba kuwa jino moja limeng'oka (Bitchuka) na jino lingine limeota (Bushoke).

Muda si mrefu, baada ya Bushoke kujiunga na OSS, hasira za aliyekuwa Katibu wa bendi hiyo, Abel Balthazar, ziliongezeka na kuamua kuwasomba wanamuziki kadhaa wa Sikinde wakiwamo Cosmas Chidumule na Fresh Jumbe.

Huko walifanya makubwa na nyimbo kama 'Kata ya Maji Ukweni', 'Ajali ya Amirani', na 'Salmada' zilifanya OSS kuwa moto.

Mwaka 1989 Bushoke aliondoka Ndekule na kujinga na bendi ya Bima Lee. Huko aliibuka na kibao kilichopendwa na wengi, 'Visa vya Mesenja.'

Ni wimbo ambao uliwashangaza wengi juu ya maudhui yake ambavyo ni aghalabu sana kutungwa pamoja na aina ya uimbaji ambao ulikuwa wa kuzungumza na kuimba pia.

Hiki ni kisa mtambuka, kinachoanzia ofisini na kumalizikia nyumbani. Kinazungumzia juu ya mesenja aliyepeleka barua za ofisini nyumbani kwa meneja. Moja ya barua ilikuwa ya mchepuko wa bosi, ikanaswa na mkewe.

Ukitafakari sana huu wimbo, utagundua kosa lilikuwa ni la meneja mwenyewe. Kuchelewesha mishahara ya wafanyakazi ndiko kulisababisha mesenja kuingia mitaani kusaka pesa kwa njia nyingine, badala ya kuwahisha barua ofisini, kiasi kwamba aliporejea akakuta ofisi zimefungwa na kuamua kuzipeleka nyumbani kwa bosi wake.

Kwa wasiofahamu, wimbo huu ulitungwa na kuanza kuimbwa kwenye bendi ya OSS, kabla ya Bushoke kuhama nao kwenda Bima Lee. Awali ulipigwa kwenye kumbi mbalimbali ambazo Ndekule walikuwa wakitumbuiza. Hebu soma kisa hiki cha kushangaza, kushtua, na kuhuzunisha kwa wakati mmoja.

"Wee Mesenjaaa. Halo sekretari eh be, eheee Mesenja yuko wapi? Sijui bosi. Mara mesenja anaibuka na kusema, naam bosi nilikuwa uani, tumbo linaniletea matatizo miye. Bosi akasema nenda posta kachukue barua za ofisini na za nyumbani, za ofisini lete ofisini na za nyumbani peleka nyumbani."

Yalikuwa mazungumzo kati ya bosi, sekretari na mesenja, yote yakiongozwa na Bushoke mwenyewe katika wimbo huo.

"Mesenja kaleta balaa nyumbani kwa meneja bila kufahamu, (kiitikio) Mesenja kaleta balaa nyumbani kwa meneja bila kufahamu. Wakati anatoka posta ofisi anawaza moyoni

mzee miye darasa la tatu la mkoloni, mke wangu na wanangu wamelalia ugali wa mhogo na chunga la kuchemsha jana, akaingia Kariakooo anaikimbiza mia wakati siku hizi mia imeota matairi. Kutoka posta ofisini akakuta ofisi imefungwa na mlangoni yupo mlinzi, akajaribu kumbembeleza apokee zile barua akakataa, akazipeleka nyumbani kwa bosi wake akamkuta

mke wa bosi akabidi azichambue kwa kuwa si desturi barua za ofisini kufika nyumbani.

Akaanza kuzichambua, kachukua ya kwanza kaweka kando, kachukua nyingine kaweka kando

kuchukua nyingine akaona mwandiko umelalia kushoto, hati kama ya kike, akaifungua neno 'darling' kama kichwa cha habari. Na baada ya kuisoma akazimia nusu saa maskini.

Siri imefichuka siri imefichuka kosa la mesenja kaleta balaa kosa la mesenja kaleta aibuuu."

Haya tena watoto wa mjini wanasema 'limeshabumbuluka.' "Alipozinduka kamkuta mwanawe mdogo amemuegemea, anasema mama nasikia njaa

Mimi sipiki leo wala sipakui, akija baba yako mwambie aje apike anawajengea wanawake majumba na kuwanunulia magari. Bosi siku hiyo alirudi saa sita usiku, kichwani ana moja moto, moja baridi. Alipogonga akaambiwa akalale huko huko kwa anaowajengea majumba na kuwanunulia magari

akabembeleza akafunguliwa mlango ile kuingia ndani, akapigwa vibao na zogo kubwa likaanza mara maneno mara kavuliwa koti mara kachaniwa shati, mesenja kaleta aibu jamaaa."

# HADITHI

## Nyuma ya Pazia-19

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKANIULIZA tukutane wapi, maana kwake hataki, mchumba wake anaweza kufika muda wowote. Nikamwambia tukutane faragha, kwenye hoteli yoyote kwa sababu wote wawili tuna mahusiano, hakuna yeyote anayetaka kuyavunja. Akaniambia niende kwenye hoteli ya Malimba kule Sinza. Nikaenda tukakutana. Ilikuwa ndani tukaongea, nikamdanganya. Mimi mtoto wa kike bwana, nikamlegeza pale akalegea mwenyewe. Baada ya kumaliza nikamuuliza, enhee walikupigia simu watekaji, wanasemaje? Na wapi safari hii?"

"Wamemwambia apeleke maeneo ya Kigamboni, kesho, awe amefika pale saa nne usiku." "Kigamboni kubwa mama, sehemu gani?"

"Amesema ukitoka barabara inayotoka feri Kigamboni, ni katikati ya msitu mdogo utokao Kibada kwenda Tuangoma mpaka Kongowe, upande wa kulia kama unakwenda Tuangoma kuna ujenzi wa kiwanda unaoendelea. Mwisho wa uzio wa kiwanda hicho kwa mbele, ndipo pesa hizo zinatakiwa kuwekwa. Na wamesema iwe saa nne usiku kwa sababu ni msitu hivi."


**********************************

Kauli tofauti za wazazi hawa zilimchanganya Eddy, hakujua nani anasema kweli nani muongo. Hakutaka kabisa kuwakutanisha kwani wao wawili hakuna hata mmoja anayejua kuwa anafahamiana na mwingine zaidi yake. Kuwakutanisha ni kuonesha kuwa kumbe anawafahamu wote na alikuwa anazuga kwa kila mmoja kuwa anamfahamu yeye tu.

Kila mmoja alifahamu kuwa mzigo ule alipewa yeye, lakini kwa ujanja wa Eddy aliutoa mzigo mmoja kwa wote wawili, kila mmoja akidhani ni kwa ajili yake.

Macky alidhani ule mzigo wa pesa alikopeshwa na alipewa kwenda kuuweka, huku Dora akidhani mzigo ule wa pesa ulikwenda kuwekwa na Eddy mwenyewe na si Macky. Badala yake Eddy alikwenda kumpa Macky ili akauweke na kutokea kilichotokea.

Simu ya mezani iliita. Mkono wake ulinyanyua kisemeo na kukiweka sikioni na mdomoni. "Bwana Eddy habari yako." Ilikuwa ni sauti nzito, iliyoshiba. Aliitambua. Ni ya Kamanda wa Polisi Kanda ya Kinondoni." "Nzuri tu kamanda shikamoo." "Marahaba. Enhee mwanangu umefikia wapi kwenye ile kazi tuliyokupa.




**"Ni kweli tumepokea watu watatu hapa. Na tumeelezwa kuwa hawa ndiyo wale ambao walikuwa wanasumbua kipindi kile ambacho tulikuwa**

Maana huku hawa watu watatu tayari akili zao zimerudi kwenye hali ya kawaida."

"Kamanda mambo yanakwenda vizuri tu. Hao jamaa kuna watu wangu watakuja kuwachukua kwa ajili ya mahojiano. Lakini tayari mambo yameshakamilika." "Yamekamilika?" "Ndiyo!" "Mtoto amepatikana? Au tayari kuna fununu alipo?" "Sio mtoto tu afande, nipe muda leo tu nikamilishe kitu, halafu kila kitu kitawekwa wazi kesho. Kuna vitu fulani nakamilisha tu kuvifuatilia, lakini kuna uwezekano mkubwa kesho nikajua mtoto yupo wapi, nani alikuwa nyuma ya huu mpango. Pia kujua ni kwa nini siri ilikuwa inavuja kila watekaji wanapotaka mzigo ukawekwe wanajua kuwa wanafuatiliwa na polisi. Mwisho kabisa afande, tutajua ni kwa nini safari hii hawakujua." "Okay, kama tayari umeshafika huko ni vizuri sana, maana wananchi wana hamu ya kujua hilo." "Kamanda, kesho kwanza nataka niongee na hawa jamaa watatu, baada ya kusailiwa na vijana wangu. Watakachoongea kinaweza kabisa kutupeleka mbele ya wahusika wote." Ahsante sana kijana, nakutakia kazi njema." Ahsante Kamanda, ila yote haya nitaongea na Mkuu wa kituo cha Polisi Kinondoni ambaye yeye na watu wake kina Chacha ndiyo walioianza hii kazi kabla ya kukabidhiwa mimi." "Okay kijana kazi nzuri." "Ahsante afande."

*********************************************

Saa tatu asubuhi kesho yake aliletewa ripoti na vijana wake waliokwenda kuwachukua wale jamaa waliowatandika kule Kigamboni na kuwapaka sumu ya kuwalevya.

Ripoti iliyoletwa na mmoja wa wasaidizi wake ilimwambia kuwa jana yake usiku waliwapeleka kwenye chumba cha mahojiano na pia kuwapa kashikashi ya kuwalazimisha waseme wao ni nani, kama walitumwa na nani alifanya hivyo na alipo mtoto aliyetekwa.

"Kiukweli bosi ni kwamba wale jamaa nao wanaonekana hawajui kitu. Tumejitahidi sana kuwabana kwa kadri tulivyoweza na mafunzo yetu, lakini tumejidhihirisha wazi kuwa hawa walitafutwa tu na kuahidiwa pesa kwa lengo moja tu la kwenda kuchukua mkoba wa pesa maeneo yale. Halafu kuna mtu walitakiwa kumpa ambaye ndiye angepeleka kwa huyo mhusika." "Duh! Hawajui lolote!!?" Eddy aliuliza na kushangaa kwa wakati mmoja." "Hakuna kitu bosi mle. Tumewarudisha rumande."

"Basi naomba waleteni hapa ofisini kwangu baada ya saa nane mchana." "Poa bosi tutafanya hivyo." Akajibu kijana msaidizi wa Eddy, aliyeonekana kuwa na umri wa miaka 24 hivi, lakini akiwa amejaa misuli.

Saa tisa na robo hivi waliletwa vijana watatu ambao kwa mbali hawakuwa wageni kwenye macho ya Eddy. Ni wale aliopambana nao maeneo ya Mikwambe, Kigamboni, Dar es Salaam.

Mmoja alimtambua kwa jina la Pius. Alilisikia wakati wenzake walipokuwa wakimtafuta. Ni wakati alipokuwa amemzimisha. Na ndiye alikuwa mtu wa kwanza kumzimisha kabla ya wale wawili.

Walionekana kuchoka kutokana na mateso ya vijana wake, ambao walikuwa kwenye juhudi za kuwalazimisha waseme hao ni nani, na wametumwa na nani.

"Enhee wewe Pius, niambie wenzako hawa wanaitwa kina nani?" Akauliza Eddy. Pius alionekana kushangaa kuitwa na mtu aliye mbele yake aliyeonekana kama mtu anayemfahamu hivi.

"Huyu anaitwa Farjala, huyu Said." Akajibu kivivu na kichovu. Wenzake walionekana kukosa amani. Nadhani walidhani wamepelekwa tena kupata adhabu. "Nimewaita hapa ili mnijibu maswali yangu machache tu ili muende mkapumzike." Hawakujibu ila walionekana kukaa tayari kwa kujibu.

"Msinidanganye. Bahati nzuri mimi mkinidanganya najua." Alisema na kuwaangalia wote kwa zamu.

"Nani aliwatuma muende Mikwambe kuchukua mkoba wa pesa?" "Malik" akajibu Pius. "Ni nani huyo?" "Yeye hakukamatwa, tulikuwa wanne, sisi tulikamatwa yeye akakimbia. Moyoni alikubali kuwa lilikuwa jibu la ukweli. Ni kweli kuna mmoja wao walimuacha akakimbia. Alikuwa na uwezo wa kumpiga na kumzimisha kama wale wengine, lakini hakutaka kufanya hivyo kwani alijua hawa aliowazimisha wangemtaja mwenzao na pia hawangesema kitu tofauti hata kama angewakamata wote.

Ila alichogundua ambacho hakuweza kukijua kabla kuwa aliyemuacha alikuwa muhimu zaidi. Angejua angehakikisha kuwa haondoki. "Aliwatumaje, au aliwaambiaje?" "Alituambia tumfuate tukachukue mkoba. Hakutuambia wa nini, ila alisema tukifanikiwa kuupata na kumkabidhi yeye, kila mmoja analipwa kiasi cha shilingi laki mbili." Farjala alidakia. "Kwa hiyo nyinyi hamkujua kwenye ule mkoba kuna nini?" "Haikuwa jukumu letu. Yeye ndiye alituongoza na kusema tuende kumsaidia kuuchukua mkoba ule muda ule wa usiku, dili likifanikiwa tunalipwa hiyo pesa." "Kwani nyinyi mnafanya kazi ya kwenda kuchukua mikoba ilipowekwa?" Wote watatu walinyamaza na kuangalia.

Kilichobainika ni kwamba vijana wake ni wahalifu ambao hufanya kazi ya kukodiwa kwenda kufanya matukio mabaya, ya kujeruhi na kuua kwa lengo la kulipwa pesa. Ndiyo maana wote walikuwa na uwezo wa kutumia silaha kama bastola na zile za jadi.

**Itaendelea Jumapili**



# KAJALA ATAMANI PAULA KUFUNGA NDOA HARAKA

MWIGIZAJI maarufu, Kajala Masanja, amesema mwanawe Paula ana haki zote za kuamua kubadili dini akifikia wakati wa kuoana na Marioo.

Amesema ndoa ni jambo la heri, na kama wakikubaliana kufunga ndoa hakuna kikwazo cha dini kwa sababu wote ni watu wazima wana haki ya kufanya maamuzi binafsi.

"Hakuna cha kuwakwamisha kwa sababu wamekaa pamoja miaka mingi na kupata mtoto. Kwangu sina tatizo nimempa uhuru Paula kuamua yeye mwenyewe kubadili dini kama anataka kufunga ndoa," amesema Kajala.

# DE MASTER KUACHIA NGOMA MPYA

**Na Halfani Chusi**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Deo Meta maarufu De Master, amesema ameamua rasmi kurudi jukwaani baada ya kimya cha muda mrefu.

De master ambeye ni mzaliwa wa Kigoma aliyeanza mziki tangu mwaka 2002, akiwa na kundi la G Mobb na kufanikiwa kurekodi wimbo mmoja uliojulikana kwa jina la Nenda Wewe ambao ulifanya vizuri kipindi hicho.

Sasa msanii huyo ameingia studio na kupika chuma kingine ambacho anatarajia kuachia audio yake leo inayokwenda kwa jina la Kichomi.

"Kichomi ni ngoma ya moto sana, ninatarajia kuipandisha audio 'youtube' kuanzia leo kwahiyo ninaomba mashabiki zangu waniunge mkono" amesema De Master



## ZISIKUPITE

### CUNHA AWA LULU ENGLAND
KLABU ya Aston Villa imejiunga kwenye mbio za kumsaka mshambuliaji wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia anazivutia klabu za Nottingham Forest, Chelsea, Arsenal, Tottenham na Manchester United ***(Mirror)***

### DORGU ATAKIWA MAN UNITED
KLABU ya Manchester United itatoa ofa ya pili kwa Lecce kwa ajili ya kumnunua beki wa Denmark, Patrick Dorgu mwenye umri wa miaka 20, baada ya dau lao la awali la pauni milioni 25 kukataliwa. (***Fabrizio Romano)***

### BARCA KUMKOSA RASHFORD
JARIBIO la Barcelona kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27 huenda likapingwa kwa kuwa hawajauza wachezaji wa kutosha ili kupata fedha. ***(ESPN)***

### BROBBEY MKATABA WA KUDUMU
KLABU ya West Ham imeambiwa itahitaji kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 22 kwa mkataba wa kudumu kwani Ajax hawana nia ya kumtoa kwa mkopo. (***Fabrizio Romano)***

### AMORIM ASIKITISHWA USAJILI
KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amesikitishwa na klabu hiyo kutokuwa na shughuli ya uhamisho huku kukiwa hakuna mchezaji aliyenunuliwa au kuuzwa mwezi huu.(***Manchester Evening News)***

### DURAN ATAKIWA SAUDI ARABIA
KLABU ya Al-Nassr ya Saudi Arabia inatayarisha ofa rasmi kwa ajili ya mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21. (***Telegraph)***

### GERNACHO KUHAMIA CHELSEA
MCHEZAJI wa Manchester United, Alejandro Garnacho atajiunga na Chelsea mwezi huu baada ya mazungumzo ya winga huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 20 kuhusu kuhamia Napoli kukwama. ***(Teamtalk***)

### KIMMICH HUYO REAL MADRID
REAL Madrid imeanza mazungumzo ya awali na kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 29, kuhusu uhamisho wa majira ya joto, mkataba wake utakapomalizika. (***Bild)***

### ARSENAL HAIJAPOKEA OFA
ARSENAL haijapokea ofa yoyote ya kumnunua mchezaji Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 28. (***Sky Sports)***

### ATLETICO YAMTAKA ZINCHENKO
KLABU ya Atletico Madrid inamtaka mchezaji wa kimataifa wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko ambaye anaweza kucheza katika safu ya ulinzi au kiungo. (***Sky Sports)***

### FERGUSON KUTIMKA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inafikiria iwapo itamruhusu mshambuliaji Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, kuondoka kwa mkopo mwezi. ***(Mirror)***

### BARCELONA YAMTAKA MURILLO
BARCELONA inamfuatilia mlinzi wa Nottingham Forest, Murillo huku Juventus na Chelsea pia wakimtaka Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 22. (***Sport)***

### CHELSEA YAIGOMEA DEPORTIVO
CHELSEA imekataa ofa ya pauni miloni 8 kwa ajili ya winga wa Deportivo La Coruna na kikosi cha vijana wenye umri wa chini ya miaka 21 cha Hispania, Yeremay Hernandez. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KIMMICH MAMBO SAFI REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

**Vigogo hao wa Hispania wameanzisha mazungumzo na nyota huyo ambaye.....**

REAL Madrid imehusishwa kutaka kumnunua kiungo wa Bayern Munich, Joshua Kimmich ambaye mkataba wake unafikia tamati mwisho wa msimu huu.

**Kimmich yuko katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Bayern, ambao hawajaficha nia yao ya kutaka kumpa mkataba mpya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.**

Hata hivyo, kumekuwa hakuna maendeleo ya kweli katika mazungumzo juu ya masharti mapya na Kimmich na sasa yuko huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild limebainisha kwamba, Kimmich anawasiliana na Madrid, ambayo inamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani.

Kikubwa zaidi, Bayern bado hawajakata tamaa ya kumbakisha Kimmich na wanapanga mazungumzo zaidi ya kuongeza muda, lakini Kimmich tayari amethibitisha kuwa hatasubiri muda mrefu zaidi kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu klabu yake ijayo.

Madrid wamekuwa wakihusishwa na Kimmich kwa muda mrefu lakini hawaoni mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kama mchezaji sahihi wa kusajiliwa kwenye mipango ya muda mrefu.

# NKUNKU KUBADILISHWA NA GARNACHO



**LONDON,** England

MANCHESTER United imeomba kufahamishwa kuhusu maendeleo kuhusu mustakabali wa Christopher Nkunku, wakati Chelsea ikiendelea kutathmini uhamisho rasmi wa Alejandro Garnacho.

Mustakabali wa Garnacho pale Old Trafford uko shakani huku Chelsea na Napoli zikiwa na nia ya kutaka kumsajili.

Licha ya Man United kubainisha kwamba hawamlazimishi Garnacho kuondoka, lakini wako tayari kusikiliza ofa.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba matamanio ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ni kujiunga na Chelsea ikiwa atalazimika kuondoka United.

Nkunku yuko tayari kuondoka Stamford Bridge mwezi huu na amekuwa akiwindwa na Bayern Munich.

Chelsea huenda ikahitaji mbadala wake ikiwa Mfaransa huyo ataondoka na wamekuwa wakihusishwa na mshambuliaji wa Bayern, Mathys Tel.

Nkunku amefunga mabao 16 katika mechi 42 kwa upande wa Ligi Kuu England.

Dakika nyingi za Nkunku msimu huu zimeingia kwenye Ligi ya UEFA Conference na ameanza mechi tatu pekee za ligi msimu huu.

United wameandaa orodha ya malengo ya nafasi kadhaa, lakini bajeti yao ndogo imemaanisha kuwa chaguzi zinazowezekana zimezuiwa.

Antony, kwa upande wake, anatazamiwa kusaini mkataba wa mkopo kwenda Real Betis hadi mwisho wa msimu huu.

# Walker ajiunga rasmi na AC Milan

**MILAN,** Italia

KYLE Walker amekamilisha uhamisho kutoka Manchester City kwenda AC Milan baada ya klabu hizo mbili kufikia makubaliano.

Walker amejiunga na timu hiyo ya Italia kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu.

Milan pia wana fursa ya kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu wa majira ya joto, lakini hakuna wajibu uliowekwa katika makubaliano hayo.

Beki huyo wa England mwenye umri wa miaka 34 ana mkataba na City hadi 2026 lakini hajashiriki katika timu hiyo tangu waliposhinda mabao 4-1 dhidi ya West Ham Januari 4.

Aliandika barua ya kuaga City kwenye Instagram baada ya uhamisho huo kuthibitishwa.

"Manchester City ... nitaanzia wapi?," Walker aliandika. "Kusaini kwa klabu hii ya aina yake mwaka 2017 ilikuwa ndoto. Miaka saba baadaye, kushinda mataji 17, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya ni kitu ambacho nilikuwa na ndoto tu kama mtoto.



"Kucheza na wachezaji wengi wenye vipaji kumenisukuma kuwa mchezaji bora zaidi kwangu, na ninashukuru sana kwa nafasi niliyoipata Etihad. Asante sana kwa wote.

"Kwa wachezaji wenzangu, tangu nilipopitia mlangoni nilijisikia kuwa nyumbani. Asante kwa kumbukumbu nzuri na mafanikio yote tuliyoshiriki pamoja. Ninyi ni marafiki, lakini pia familia ya maisha. Kwa Pep Guardiola, asante kwa kuniamini.

"Mwisho, kwa mashabiki, asanteni kwa kunikumbatia kama mmoja wenu tangu siku ya kwanza. Usaidizi wenu usioyumba."

Kuondoka kwa Walker kunamwacha Guardiola kukosa mabeki wa kulia wanaotambulika licha ya kusajiliwa kwa mabeki wawili wapya mwezi huu.

Abdukodir Khusanov kutoka Lens na Vitor Reis mwenye umri wa miaka 19 kutoka Palmeiras wote wamejiunga na City kwenye dirisha la Januari.

Uhamisho wa Walker kwenda Milan unamaliza nafasi ya Marcus Rashford kwenda San Siro.

Milan walikuwa wameonesha nia ya kutaka kumnunua Rashford, lakini sheria za Serie A kuhusu kusainiwa kwa wachezaji wasio wanachama wa Umoja wa Ulaya inamaanisha kwamba nafasi yoyote ya kufikiwa kwa makubaliano hayo imekufa.

Walker anaondoka City akiwa ameshinda mataji sita ya Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipoondoka Tottenham Hotspur mwaka 2017.

# Maresca: Palmer ndio Mo Salah wetu

**LONDON,** England

KOCHA mkuu wa Chelsea, Enzo Maresca amelinganisha ushawishi wa fowadi, Cole Palmer kwenye timu na ule wa mfungaji bora wa Ligi Kuu England, Mohamed Salah kwa Liverpool.

Palmer alijiunga na klabu hiyo ya London Magharibi akitokea Manchester City Septemba 2023 na amekuwa mchezaji bora tangu wakati huo, akifunga mabao 22 katika ligi msimu uliopita chini ya Mauricio Pochettino na kuongeza mengine 14 kwenye jumla ya mabao hayo msimu huu, pamoja na asisti sita.

Huku Salah akiwa kileleni mwa orodha ya wafungaji wa ligi msimu huu akiwa amechangia mabao 18 na asisti 13 na kusaidia Liverpool ya Arne Slot kuweka pengo la pointi sita kileleni mwa ligi ikiwa na mchezo mkononi.

"Yeye (Palmer) anaimarika sana lakini sio tu kwa idadi ya mabao na asisti," alisema Maresca katika mkutano wake na waandishi wa habari jana.

"Kipindi cha pili dhidi ya Wolves kwangu kilikuwa moja ya wakati mzuri zaidi tangu niwasili hapa. Alikuwa anaonesha utu, alikuwa akiomba mpira wakati wowote ambao timu iliuhitaji.

"Liverpool wanapokuwa na nyakati ngumu Salah anaomba mpira. Arsenal wanapokuwa na tatizo fulani, Martin Ødegaard anaomba mpira.

"Tunahitaji mchezaji wa aina hiyo tunapokuwa katika nyakati ngumu, ambaye anawageukia wachezaji wenzake na kusema: 'Nipe mpira, usijali, nitakuwa msimamizi.'

"Aina hii ya utu ambayo tunapaswa kuonesha katika wakati mgumu. Dhidi ya Wolves kipindi cha pili alikuwa juu."



# MTIBWA YASHINDA MECHI 5 MFULULIZO

**Na Adam Fungamwango**

MTIBWA Sugar, juzi ilipata ushindi wa tano mfululizo kwenye Ligi ya Championship, ilipoifunga Green Warriors mabao 2-1 katika mchezo wa raundi ya 16, uliochezwa Uwanja wa Mabatini, Pwani na kuzidisha matumaini ya kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

Ushindi huo unakuwa wa tano mfululizo baada ya awali ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Biashara United, Novemba 15 mwaka jana kwenye Uwanja wa Karume, Mara.

Baada ya hapo ilipata ushindi dhidi ya TMA, mabao 2-1, Mbuni FC 2-0, Mbeya Kwanza 2-1, Bigman bao 1-0, kabla ya mchezo wa juzi.

Straika hatari wa timu hiyo, Raizin Hafidh, aliendeleza kasi yake ya kufunga mabao kwenye ligi hiyo alipotupia bao la kwanza dakika ya 18 lililomfanya kufikisha mabao 12, akiwa kileleni kwenye orodha ya wafungaji katika ligi hiyo.

Wenyeji walisawazisha dakika ya 43, kabla ya Erick Kyaruzi kufunga bao la pili, dakika tano baadaye.

Ushindi huo unaoifanya timu hiyo iliyoshuka daraja msimu uliopita, kufikisha pointi 41 ikiwa juu ya msimamo wa ligi, ikishinda michezo 13, sare mbili na kupoteza mchezo mmoja.

Aidha, kipigo cha juzi kinaifanya Green Warriors kusalia na pointi zake 11, ikiwa kwenye nafasi ya 12 katika msimamo.

Katika mechi nyingine iliyochezwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona Mkoani Mtwara, Mbeya Kwanza iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Songea United.

Ushindi huo unaisogeza Mbeya Kwanza hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikifikisha pointi 30 baada ya michezo 16 huku Songea United ikibaki nafasi ya saba na pointi zake 24.

Mchezo mwingine uliochezwa Uwanja wa Kituo cha TFF, Mnyanjani, Tanga, wenyeji African Sports iliiadhibu Cosmopolitan mabao 2-1.

African Sport sasa imefikisha pointi 11, ikiwa nafasi ya 11, huku Cosmo, Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1967, inashika nafasi ya 14, ikiwa na pointi tisa.




Meneja wa wateja maalum wa kampuni ya Yas, Mary Rutta (wa tatu kutoka kulia) akiwa na washindi wa magifti kwenye picha ya pamoja juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Barrick kusaidia kuinua michezo

**Na Faustine Feliciane,**
aliyekuwa KAHAMA

KAMPUNI ya uchimbaji dhahabu ya Barrick imepanga kusaidia ukuaji wa michezo katika maeneo yanayozunguka migodi yake ya North Mara mkoani Mara na Bulyanhulu mkoani Shinyanga.

Akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari kwa ajili ya kutoa ripoti ya kampuni hiyo, Meneja Mkuu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Victor Lule, alisema wamepanga kuhangia ukuaji wa michezo kuanzia ngazi ya chini na kwa sasa wapo kwenye mchakato wa ndani kuanza programu hiyo.

"Tayari tumeanza huu mchakato, tunataka kuinua michezo kuanzia ngazi ya chini kabisa, tunafahamu michezo inaleta ushirikiano na mahusiano mazuri, tunajipanga kufanya hivyo," alisema Lule.

Lule alitoa ufafanuzi huo baada ya kuulizwa ni namna gani kampuni hiyo inasaidia kwenye sekta ya michezo.

Awali, mbunge wa jimbo la Msalala, Iddi Kassim, aliomba kampuni hiyo kuisaidia timu ya Bulyanhulu 'Buly FC' inayoshiriki ligi za chini ili iweze kupanda mpaka ngazi za juu.

"Tunafahamu kuna mkakati wa vijiji 16 katika kuendeleza michezo, lakini niombe pia tuna timu yetu ya eneo hili, tunaomba ipewe udhamini ili iweze kufanya vizuri, na hii timu imebeba jina la mgodi," alisema Iddi.

Kwa upande wake, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow, alisema wataangalia namna bora ya kusaidia michezo katika maeneo yanayozunguka migodi ya kampuni hiyo ikiwa pamoja na kutengeneza miundombinu.

## Pamba Jiji: Unyonge mwisho mzunguko wa kwanza tu

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Pamba Jiji, imeeleza kufurahishwa na usajili ilioufanya kwenye dirisha dogo la uhamisho lililofungwa Januari 15 mwaka huu huku ikiwa na matumaini ya kufanya vyema mechi zijazo na kuja na kauri mbiu ya 'unyonge mwisho mzunguko wa kwanza.'

Ofisa Habari na Klabu hiyo, Moses William, amesema jana kuwa wameridhishwa na usajili walioufanya kwa kuongeza wachezaji bora ambao wataleta ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza, Februari Mosi.

Pamba inatarajiwa kucheza mechi ya raundi ya 17, Februari 5 mwaka huu dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Kikosi hicho tayari kimeshaingia kambini kujiandaa na mchezo huo pamoja na mechi zinazofuata za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

"Mechi dhidi ya Dodoma Jiji, haitokuwa mechi rahisi, haitokuwa mechi ya kizembe, lakini sisi kama Pamba Jiji tumejindaa vizuri kwenda kutoa burudani. Tunasema hivi, kwa usajili huu ambao tumeufanya kwenye dirisha dogo, ukiunganisha na kazi inayofanywa na benchi la ufundi, tunasema hivi..., unyonge mwisho mzunguko wa kwanza," alisema.

Pamba jiji imesajili wachezaji 11 kwenye dirisha dogo, kuelekea mechi za mzunguko wa pili, ambao ni Deus Kaseke, Habib Kyombo, Hamad Majimengi, Cherif Ibrahim kutoka Cameroon, na Zabona Mayombya.

Wengine ni kiungo mshambuliaji wa timu ya taifa ya Burundi, Shassir Nahimana aliyesajiliwa kutoka Tuskera ya Kenya ambako alikuwa nahodha, kipa raia wa Sierra Leone, Mohamed Kamara, straika Mcameroon, Francois Bakari, Mathew Tegis kutoka Shabana ya Kenya, kiungo mshambuliaji kutoka Guinea, Abdulaye Camara na beki wa kati Mgambia, Modou Camara.

# Michezo

Jumapili Januari 26, 2025

Nipashe




Maresca: Palmer ndio Mo Salah wetu UK. 21

# Hasira Yanga zaishia Copco FC

## ●●● Yaiangushia mzigo wa magoli kwenye harakati za kutetea ubingwa wa....



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahaya (kushoto) akijaribu kumtoka beki wa Copco FC, Amos Mgeta huku Jonas Mkude akiwa karibu wakati wa mchezo wa Kombe la FA jana kwenye uwanja wa KMC, Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

**Na Adam Fungamwango**

HASIRA za Yanga kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, jana zilishia kwa Copco FC, ilipoibugiza mabao 5-0 katika mchezo wa raundi ya tatu Kombe la FA uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

**Mabao ya Yanga kwenye mchezo huo yalifungwa na Shekhan Ibrahim, Prince Dube, Maxi Nzengeli, Duke Abuya na Mudathir Yahaya.**

Copco, yenye maskani yake jijini Mwanza ilionekana kuidhibiti Yanga kipindi cha kwanza iliporuhusu bao moja tu, lakini ilishindwa kabisa kufanya hivyo kipindi cha pili na kuruhusu mvua ya mabao.

Katika mchezo huo, ilishuhudiwa Yanga ikimchezesha kwa mara ya kwanza beki wake, Israel Mwenda huku Jonas Mkude akianza kipindi cha kwanza kama beki wa kati.

Yanga ilifanikiwa kupata bao la kwanza dakika ya 35 lililofungwa kwa kichwa na Shekhan aliyeruka juu mbele ya wachezaji watatu wa Copco na kupiga kichwa mpira wa kona uliopigwa na Farid Mussa lililodumu hadi mapumziko.

Kwa dakika zote 45 za kwanza, kipa wa Yanga, Aboutwalib Mshery ni kama alikuwa yuko likizo, kwani alidaka mpira mara mbili tu ambayo yote haikuwa na madhara yoyote.

Kazi nzuri iliyofanywa na Mkude akipeleka mpira kwa Mwenda ambaye aliupiga mpira mrefu kwa Dube ilizaa bao lililofungwa na Mzimbabwe huyo baada ya kumtoka beki, Amos Mgeta na kuukwamisha mpira wavuni dakika ya 57.

Nzengeli aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Abobakar Salum alifunga bao la tatu kwa mkwaju wa penalti dakika ya 68, baada ya yeye mwenyewe kuangushwa ndani ya eneo la hatari.

Kama vile haitoshi, Abuya alipachika bao la nne kwa kichwa akiunganisha krosi kutoka wingi ya kushoto iliyomiminwa na Nickson Kibabage dakika ya 77, kabla ya Mudathir ambaye naye aliingia kipindi cha pili kupigilia bao la tano akifunga pia kwa kichwa kufuatia krosi ya Mwenda.

Yanga walikuwa na nafasi ya kupata ushindi mkubwa zaidi kama kiungo wake Aziz Ki angezitumia vyema nafasi alizopata katika dakika za 14 na 15.

Matokeo hayo sasa yanaitupa nje ya mashindano Copco FC huku Yanga ikisonga mbele.

# Simba: Tutacheza kama fainali leo

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola amesema wataingia kwenye mchezo wa raundi ya tatu, Kombe la FA dhidi ya Kilimanjaro Wonders kucheza kama fainali, kwani hawataki yawatokee kama ilivyokuwa kwa Mashujaa FC, na Green Worriors miaka kadhaa nyuma.

Akizungumza kuelekea kwenye mchezo huo dhidi ya timu hiyo inayoshiriki Ligi ya Mkoa Kilimanjaro, Matola alisema hawawezi kusahau kile kilichowatokea miaka ya nyuma hivyo wataingia kamili kwenye mchezo huo.

"Tumejipanga vizuri na mchezo huu kwa sababu ni mechi ya mtoano, siku zote aina hizi za mechi zimekuwa hazina mwenyewe, ukikosea tu uko nje ya mashindano, kutokana na hilo tunauchukua huu mchezo kwa umuhimu mkubwa.

Tunakwenda kucheza mechi hii kama tunakwenda kucheza fainali kwa sababu tuna uzoefu na mashindano haya, tena na timu kama hizi zimeshawahi kututoa si mara moja kwa hiyo tunaichukulia kwa umuhimu mechi ya kesho, tunakwenda kucheza kama ni mchezo wa mwisho wa fainali."

Simba iliwahi kutolewa kwenye hatua za mwanzo, Desemba 22, 2017, dhidi ya Green Warriors kwa penalti 4-3, baada ya kumaliza dakika 90 kwa sare ya bao 1-1 kabla ya kujirudia Desemba 26 kwenye uwanja huo huo wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ilipotolewa kwenye raundi ya tatu kwa mabao 3-2, dhidi ya Mashujaa FC, iliyokuwa Ligi Daraja la Kwanza wakati huo.

Mashabiki wa Simba leo wanatarajiwa kumiminika kwa wingi, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, uliopo maeneo ya Mwenge saa 10:00 jioni kuona timu yao baada ya kuzuiwa, Jumapili iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam katika mchezo wa mwisho wa makundi Kombe la Shirikisho, dhidi ya CS Constantine ya Algeria baada ya kufungiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kufuatia vurugu zilizojitokea kwenye mchezo wao dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia uliochezwa kwenye uwanja huo huo, Desemba 15 mwaka jana.

Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Wonders, Daud Macha 'Ndailagije', alisema wataingia uwanjani kwa ajili ya kupambana na timu kubwa, nzuri ya Simba kwa kuiheshimu.

"Tumekuja kwa ajili ya kupambana kwenye mchezo huu, kikosi kipo vizuri, staili yetu ya kucheza ni ya kawaida tu, tunaiheshimu Simba kwa sababu ni timu kubwa.

Hatutarajii makubwa sana kwenye mchezo huu, lakini huu ni mchezo wa mpira, hatuwezi kusema tumekuja kwa ajili ya kushindwa, tumekuja kwa ajili ya kujifunza na kupambana pia," alisema.

Msimu uliopita, Simba ilitolewa katika hatua ya 16 bora dhidi ya Mashujaa FC kwa penalti 6-5, mechi ikichezwa, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, baada ya timu hizo kumaliza dakika 90 kwa kufungana bao 1-1.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >